SportPesa
TZS. 468,576,020
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**WATUMISHI** 1,490 waliotimuliwa serikalini kulipwa stahiki zao

UK.4




KUFUNGA UBALOZI DAR...

**Wanadiplomasia wanaponusa uwezekano athari uwekezaji**



UKURASA 11

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumatano Septemba 1, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580690

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710

# Gwajima njiapanda



**Bunge** lataka vyombo vya dola, CCM kumshughulikia, awaweka mawaziri, vigogo mtegoni, yeye na Silaa wasimamishwa kwa...

*Uk. 2 & 3*





Mbunge wa Jimbo la Ukonga, Jerry Silaa (katikati), akisindikizwa na askari kutoka nje ya ukumbi wa Bunge, jijini Dodoma jana, baada ya kupewa adhabu ya kutohudhuria mikutano miwili ya Bunge. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Mawakili Mbowe wapinga uhalali wa mahakama ya mafisadi

UKURASA 4

## Kilio cha wananchi chasikika, tozo miamala simu yashushwa

UK. 3

**MICHEZO** SIMBA DAY NI AL AHLY, MAMELODI KWA MKAPA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

# Corona yapangua muda vikao vya bunge

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ametangaza kupangua ratiba ya vikao vya Mkutano wa Nne wa Bunge la 12 ulioanza jana kutokana na baa la corona.

Amesema watu wote watakaoingia kwenye Ukumbi wa Bunge watapaswa kuwa wamevaa barakoa isipokuwa wenye matatizo yanayowazuia kuvaa vifaa hivyo, lakini lazima kuwe na uthibitisho wa wataalamu.

Katika kuhakikisha kunakuwa na tahadhari dhidi ya virusi hivyo, kiongozi huyo amesema idadi ya wabunge watakaoingia ukumbini itapunguzwa na hakutakuwa na wageni bungeni, isipokuwa waandishi wa habari na maofisa wa serikali watakaofika kwa kazi maalum.

Spika Ndugai alitangaza utaratibu huo jana bungeni, akibainisha kuwa baadhi ya wabunge watalazimika kushiriki vikao vya Bunge wakiwa kwenye Ukumbi wa Msekwa na watapata haki zote ikiwa ni pamoja na kuuliza maswali na kuchangia hoja.

Spika Ndugai pia alisema muda wa kipindi cha 'Maswali' umepunguzwa kutoka saa moja na nusu hadi saa moja na vikao vya jioni sasa vitakuwa vinaanza saa 8:00 mchana hadi saa 1:00 usiku.

Kutokana na taarifa hiyo ya Spika, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisimama na kuliomba Bunge liazimie kutengua kanuni zake, ili kuridhia utaratibu mpya wa ratiba za vikao vya chombo hicho cha kutunga sheria.

Virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19 viliripotiwa kwa mara ya kwanza Wuhan, China Novemba 2019 na Tanzania iliripoti kupata mgonjwa wa kwanza Machi 16 mwaka jana.

# Askofu Gwajima njiapanda

**Na Sanula Athanas,**
DODOMA

NI njiapanda! Ndivyo unavyoweza kusema kutokana na azimio la Bunge dhidi ya Mbunge wa Kawe, Josephat Gwajima.

Baada ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kumtia hatiani kwa utovu wa nidhamu, jana Bunge lilipitisha azimio la kumfungia kushiriki mikutano miwili ya chombo hicho.

Bunge pia liliazimia vyombo vya dola vichukue hatua kutokana na kauli zilizotolewa na Gwajima na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilichompa ridhaa ya kuwa mbunge, kimwajibishe kwa mujibu wa taratibu zake za ndani ya chama.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Emmanuel Mwakasaka, alitumia dakika 38 kuanzia saa 4:36 asubuhi kuwasilisha bungeni taarifa yao kuhusu shauri la Askofu Gwajima, akisisitiza mbunge huyo hakutoa ushirikiano kwa kamati.

Kwa mujibu wa Kamati ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, Gwajima alihojiwa na kamati kuhusu kauli zake alizozitoa Julai 25, 2021, Agosti Mosi, 2021 na Agosti 15, 2021 akiwa maeneo ya Ubungo mkoani Dar es Salaam.

Alisema mbunge huyo alifika mbele ya kamati kuhojiwa na alikiri kutoa kauli zinazolalamikiwa zilizosambazwa kwenye mitandao ya kijamii, akisisitiza ni mahubiri yake kanisani na hayapaswi kuhojiwa bungeni.

Mwakasaka alisema kutokana na kauli hiyo ya Gwajima, kamati ililazimika kurejea Ibara 19 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 kuhusu uhuru wa kuabudu ambayo imeelekeza masuala ya kuabudu kuzingatia sheria za nchi ili kulinda maadili katika jamii.

"Kamati ilijiridhisha mahubiri yanayotolewa yanapaswa kulinda usalama na maadili kwa jamii na tuliporejea Ibara ya 30 ya Katiba hiyo, tulibaini hakuna kinga ya mahubiri ya kanisani kuhojiwa.

"Mheshimiwa Josephat Gwajima ni mbunge na askofu. Anapaswa kuwa mfano bora kwa jamii. Kamati imejiridhisha kuwa kauli za Mheshimiwa Gwajima zinadhalilisha Bunge na kuchonganisha mihimili. Kauli hizi ni utovu wa nidhamu uliokithiri," alisema.

Mwakasaka aliendelea kubainisha kuwa akiwa mbele ya kamati, Gwajima alionyesha kuwa mtu mwenye jeuri na kejeli kwa kamati na alishindwa kuthibitisha kauli zake na hakuwa na kielelezo chochote licha ya kuwaaminisha wananchi kwamba anao ushahidi kuhusu kilicho nyuma ya chanjo ya corona.

"Mheshimiwa Gwajima alishindwa kuthibitisha viongozi kupewa rushwa ili kuidhinisha chanjo ya corona aina ya Johnson & Johnson na hivyo kamati ilimtia hatiani.

"Shahidi Gwajima alipofika mbele ya kamati na kukataa kutumia kiti kilichoandaliwa, akakataa kutumia kipaza sauti na hata kufikia hatua ya kuhojiwa akiwa amesimama. Kamati iliamua kumvumilia.

"Gwajima hakutoa ushirikiano kwa kamati na kwenye maeneo mengi, hata yaliyohitaji majibu mafupi, alielezea masuala ya imani yake na kujivunia idadi kubwa ya waumini wake waliopo maeneo mbalimbali duniani," alisema.

Mwakasaka alisema kamati yao katika kufuatilia mwenendo wa shahidi huyo, ilibaini ni mkaidi na jeuri na hakutaka kujutia kauli zake licha ya kuwa zinachonganisha mihimili na kupotosha wananchi.

Kamati hiyo ilipendekeza Askofu Gwajima apewe adhabu hiyo ya kutoshiriki mikutano miwili ya Bunge na vyombo vingine vichunguze kauli zake zenye mwelekeo wa uchochezi na upotoshaji.

Pia ilipendekeza Gwajima achukuliwe hatua na chama kilichompa ridhaa ya kuwa mbunge, CCM. Bunge liliridhia azimio hilo.

Kutokana na kusimamishwa kushiriki shughuli za Bunge, Spika Ndugai alitangaza kuwa Gwajima na Mbunge wa Ukonga, Jerry Silaa (CCM), watakuwa wanalipwa nusu ya mishahara na posho zingine za kibunge kwa kipindi chote cha adhabu kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge.

# ...Awaweka mtegoni mawaziri, vigogo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge imemwomba Spika kuidhinisha Mbunge wa Ukonga (CCM), Jerry Silaa, akamatwe kwa kukaidi kufika kuhojiwa kwa mara ya pili na kamati hiyo.

Kutokana na mbunge huyo kutofika mbele ya kamati hiyo jana, imemwomba Spika Ndugai kutoa kibali cha kukamatwa na kumfikisha mbele ya kamati leo saa nne asubuhi.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Emmanuel Mwakasaka, alisema jana kuwa shahidi huyo alipaswa kufika mbele ya kamati hiyo jana saa tano asubuhi lakini hakufika na hakutoa taarifa yoyote ya kutofanya hivyo.

"Leo (jana) tulikuwa tunaendelea na shauri la Mheshimiwa Silaa ambaye hajafika mbele ya kamati hii na hatuna taarifa yoyote ya kwa nini hatofika kwenye kamati hii.

"Sasa sisi kwa mujibu wa kanuni na sheria ambazo ni za Haki, Kinga, Maadili na Madaraka ya Bunge, Mheshimiwa Spika yeye ndiye mleta shauri. Kwa hiyo, kwa kutumia sheria hizo nimeomba kibali kwa Spika ili akamatwe na kuletwa hapa kama sheria zetu zinavyoturuhusu,"alisema.



Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, Emanuel Mwakasaka akiwasilisha taarifa ya mahojiano waliyowahoji Mbunge wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima na Mbunge wa Ukonga, Jerry Silaa, kwenye mkutano wa nne wa Bunge jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

Mwakasaka alisema Spika akiridhia, shahidi huyo atapelekwa mbele ya kamati kwa mujibu wa sheria.

"Sisi tulimwita ili tuendelee na shauri lake maana juzi tulimwita na kwa kawaida anaendelea na kiapo chake kilekile, tumemsubiri kwa muda wa kutosha lakini hakuna taarifa yoyote," alisema.

Alibainisha kuwa kwa mujibu wa sheria, kwa kuwa mbunge huyo hakupeleka taarifa, hati ya kukamatwa inapaswa kuandaliwa.

"Kwa hiyo sisi kama kamati tumemwomba Mheshimiwa Spika, tunasubiri kibali chake ili ikiwezekana kesho (leo) saa nne asubuhi aweze kuletwa hapa na vyombo vinavyohusika na mambo ya usalama.

"Kibali cha kukamatwa hutolewa hata mahakamani kwa yule aliyepewa jukumu la kumkamata huyo mtu muda wowote. Sasa anahifadhiwa wapi hadi kuletwa eneo la mahojiano hilo linakuwa chini ya watu wa usalama," alisema.

Agosti 23, mwaka huu, mbunge huyo alifika mbele ya kamati hiyo kufuatia wito wa Spika kutokana na tuhuma mbalimbali zinazomkabili ikiwamo kusema uongo na kushusha hadhi na heshima ya Bunge.

Agosti 21, mwaka huu, Spika Ndugai aliagiza mbunge huyo kufika mbele ya kamati kwa mujibu wa kanuni ya 4(1) (a) na (b) ya nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Juni 2020 ambayo inaipa mamlaka kamati hiyo kuchunguza mambo yanayohusu maadili ya wabunge yanayopelekwa kwa Spika.

# Kilio cha wananchi chasikika, tozo miamala simu yashushwa

**Na Elizabeth Zaya**

HATIMAYE serikali imetangaza kupunguza tozo za miamala ya simu kwa asilimia 30.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari jana na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano, Wizara ya Fedha na Mipango, Benny Mwaipaja, tayari punguzo hilo limesainiwa kwa ajili ya utekelezaji.

"Julai 19, 2021, Rais Samia Suluhu Hassan, aliwaelekeza Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba na Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, kupitia upya tozo za miamala ya simu baada ya kusikia kilio cha wananchi kuhusu tozo hizo," ilieleza taarifa hiyo.

"Katika kutekeleza maelekezo hayo, leo Agosti 31, 2021 Waziri Nchemba, ametia saini marekebisho ya Kanuni za Tozo za Miamala ya Kielektroniki za kutuma na kutoa fedha za mwaka 2021 na kupunguza viwango vya tozo za miamala hiyo kwa asilimia 30."

"Aidha, serikali imefanya majadiliano na watoa huduma za simu ambao nao wameridhia kupunguza viwango vya tozo wanazotoza katika miamala ya kutuma na kutoa fedha kati ya mtandao na mtandao mwingine kwa asilimia 10," taarifa ilieleza.

Kwa mujibu wa taairifa hiyo, viwango vilivyopunguzwa vitatangazwa rasmi kupitia Gazeti la Serikali leo.

"Serikali inaamini kuwa uamuzi huo utatoa nafuu kwa wananchi na kuiwezesha serikali kupata fedha za kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kama ilivyokusudiwa wakati tozo hizo ziliporidhiwa na kupitishwa na Bunge la Bajeti la Mwaka 2021/2022," taarifa hiyo ilieleza zaidi.

"Ni imani ya serikali kwamba wananchi wataunga mkono uamuzi huu, kwani tozo hizo zimeanza kuleta manufaa makubwa kwa wananchi ikiwamo kiasi cha Sh. bilioni 48.4 zilizokusanywa hivi karibuni ambazo zimeelekezwa katika kujenga vituo vya afya 150 na ukamilishaji wa vyumba vya madarasa 560 nchi nzima."

# Spika amtaka Silaa aombe radhi

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MBUNGE wa Ukonga, Jerry Silaa (CCM), amesimamishwa kushiriki mikutano miwili ya Bunge huku Spika Job Ndugai akimtaka aombe radhi hadharani.

Uamuzi huo uliridhiwa na Bunge jana baada ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuwasilisha taarifa yake kuhusu shauri dhidi ya mbunge huyo ikimtia hatiani kwa kauli yake kwamba 'mishahara ya wabunge haikatwi kodi'.

Bunge pia limeridhia mbunge huyo avuliwe uwakilishi wake kwenye Bunge la Afrika (PAP) kwa madai anaweza kusema uongo huko.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Emmanuel Mwakasaka, alitumia dakika 28 kuanzia saa 5:42 asubuhi kuwasilisha bungeni jijini hapa taarifa ya kamati kuhusu shauri dhidi ya mbunge huyo aliyewahi kuwa Meya wa Jiji la Dar es Salaam.

Mwakasaka aliliambia Bunge walipata wasaa wa kufuatilia mwenendo wa shahidi huyo mbele ya kamati na kubaini ni mkaidi, jeuri na hakutaka kujutia kauli zake licha ya kuitwa mbele ya kamati hiyo.

Alisema Silaa, akizungumza na wananchi wa Ukonga, alitoa kauli kwamba wabunge hawalipi kodi katika mishahara yao, jambo lililopingwa kwa kuwa wabunge wanakatwa kodi katika mishahara yao.

"Mheshimiwa Silaa alikiri kutoa kauli hiyo alipokuwa anahutubia wananchi wa Ukonga. Alikiri mbele ya kamati kuwa kwenye mshahara wake wa ubunge kuna kiasi kinakatwa kodi na kingine hakikatwi kodi.

"Mheshimiwa Silaa aliiambia kamati kwamba posho za wabunge hazikatwi kodi. Kinachokatwa ni 'basic salary'," alisema.

Mwakasaka alibainisha kuwa kamati ilimhoji Mhasibu Mkuu katika Sekretarieti ya Bunge ambaye alikiri mishahara ya wabunge inakatwa kodi lakini posho za watunga sheria hao hazikatwi kodi na kwamba utaratibu huo wa kutokata kodi kwenye posho unatumika maeneo mengine serikalini.

Alisema shahidi huyo aliikabidhi kamati hati ya mshahara wa Silaa na kutumika kama moja ya vielelezo vya shauri hilo.

"Tumeona Mheshimiwa Silaa alikuwa na nia ovu ya kuchonganisha Bunge na wananchi. Kitendo hicho ni utovu wa nidhamu uliokithiri.

"Kamati ilipata wasaa wa kufuatilia mwenendo wa Mheshimiwa Silaa mbele ya kamati na kubaini hakuwa tayari kujibu maswali kikamilifu. Kwa kifupi, shahidi hakutoa ushirikiano kwa kamati.

**TUHUMA NZITO**

Mwakasaka alisema Silaa aliandika barua kwa Katibu wa Bunge akiituhumu kamati kutomtenda haki na shauri lake liliendeshwa kwa upendeleo.

"Barua yake ilikuwa na maneno makali dhidi ya kamati. Kwenye barua yake alisema hatafika mbele ya kamati kwa sababu hakupatiwa taarifa ya wito na akahoji kwa nini kamati umulize kama anafaa kuwa mbunge wa PAP na uvumilivu wake umefika mwisho, hivyo atashtaki kwenye mahakama ya umma.

"Tulijiridhisha huyu mbunge kwa mwenendo wake huu, atasema uongo kwenye Bunge la Afrika (PAP). Tunapendekeza Bunge liazimie asimamishwe kuhudhuria mikutano miwili ya Bunge na aondolewe kuiwakilisha nchi katika Bunge la PAP," Mwakasaka aliwasilisha.

**AOMBE RADHI**

Spika wa Bunge, Job Ndugai, alisema kitendo cha mbunge huyo kulichafua Bunge mbele ya jamii kwamba wabunge hawalipi kodi, hakikubaliki na anapaswa kuomba radhi hadharani.

"Lazima aombe radhi kwenye 'public' kuhusu hili suala la kudhalilisha wabunge. Hatujaomba ubunge ili kuvunjiwa heshima," aliagiza.

Spika Ndugai alisema kuwa kwa nchi za Magharibi, mtu akitajwa kuwa mkwepaji wa kodi za serikali, anaweza kuchukua uamuzi mgumu, ukiwamo wa kujinyonga.

"Adhabu hizo ni ndogo sana, basi tu kwa sababu hawa ni ndugu zetu. Gwajima hayupo. Silaa yupo humu ndani. Sasa kwa heshima ninakutaka uondoke humu bungeni, tukutane mkutano wa Januari. Na askari hakikisheni mnamsindikiza hadi nje kabisa ya viwanja vya Bunge," Spika aliagiza.



Mbunge wa Jimbo la Dodoma, Anthony Mavunde, akichangia hoja kwenye kikao cha kwanza cha Bunge la Nne, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wabunge watumia Biblia kumjadili Gwajima bungeni

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WABUNGE wote waliohudhuria kikao cha Bunge jijini Dodoma jana, waliridhia azimio la Bunge kuwasimamisha kuhudhuria mikutano miwili Mbunge wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima na Mbunge wa Ukonga, Jerry Silaa.

Baadhi ya wabunge walinukuu mistari ya Biblia, wakidai kusikitishwa na kauli zilizowatia hatiani wabunge wenzao hao.

Wiki iliyopita Gwajima na Silaa waliitwa na kuhojiwa na Kamati ya Kinga, Maadili na Madaraka ya Bunge kutokana na kutuhumiwa kutoa kauli zilizolalamikiwa kushusha hadhi na heshima ya Bunge.

Mara tu baada ya kuwasilishwa kwa taarifa kuhusu shauri dhidi ya wabunge hao jana, Mbunge wa Kilindi (CCM), Omary Kigua, amesema ujio wa Askofu Gwajima kwenye kamati kujibu shauri ulikuwa wa dharau na kejeli.

Kigua ambaye ni mjumbe wa kamati hiyo alisema walishuhudia vituko katika kamati hiyo na vitendo vya mbunge huyo havifanani na nafasi aliyonayo.

"Shahidi (Gwajima) hakuitendea haki, hakuwa na nidhamu, heshima na hata ujio wake katika kamati ulikuwa wa dharau na kejeli zilizopitiliza," alilalamika Kigua.

Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Sophia Mwakagenda, alimtaka Askofu Gwajima kuacha tabia ya kukwamisha waumini wake kiimani na asiwadanganye wananchi.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mariam Ditopile, alisema Askofu Gwajima anapaswa kupewa adhabu ya kuvuliwa ubunge kwa madai kuwa amefanya uhaini.

Kuhusu Silaa, Sophia alisema wabunge vijana wamechoka na vituko vyake vya kuwazungumzia uongo wabunge na kwamba ametia doa usomi wake na anapaswa kuomba radhi.

Mbunge wa Singida Magharibi (CCM), Elibariki Kingu, akinukuu baadhi ya mistari iliyoko kwenye Biblia, alisema Askofu Gwajima amekuwa akipotosha kuhusu chanjo, hasa baada ya kifo cha Rais John Magufuli, jambo ambalo sio zuri.

# Watumishi 1,490 waliotimuliwa kulipwa stahiki

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema inaandaa malipo ya stahiki za watumishi 1,491 walioondolewa kwenye orodha ya malipo ya mishahara kwa kukosa sifa ya kurejeshwa kwenye utumishi wa umma kutokana na kushindwa kujiendeleza kielimu.

Watumishi hao ni wenye elimu ya darasa la saba ambao waliajiriwa baada ya tangazo la serikali Mei 20, 2004 na walipaswa kujiendeleza kielimu ili kuwa na elimu walau ya kidato cha nne kufikia Desemba, 2020.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, alisema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Geita Vijijini (CCM), Joseph Musukuma.

Katika swali lake, Musukuma alisema pamoja na serikali kutoa waraka, asilimia 95 ya watumishi hawajalipwa na kumtaka waziri kuwapa orodha ya watumishi hao ili wabunge wawatetee na kupata stahiki zao.

Akijibu swali hilo, Ndejembi alisema Rais Samia Suluhu Hassan alitoa maelekezo kwamba watumishi 1,491 stahiki zao zilipwe.

"Tayari Ofisi yetu ya Utumishi ilishatoa Waraka Mei 21, 2021 kwa waajiri wote kuanza kuhakiki madeni haya na kuanza kuangalia stahiki walizotakiwa kulipwa hawa wa darasa la saba na baada ya muda mfupi wataanza kulipwa hao 1,491," alisema.

Aliwataka waajiri kukamilisha utekelezaji wa maelekezo hayo kwa haraka na kwa usahihi ili watumishi husika wapate haki zao mapema.

Ndejembi alisema kwa wale ambao hawakupata taarifa popote kwamba wajiendeleze na walijiendeleza kabla ya muda uliowekwa waajiri wote nchini waliangalie suala hilo.



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza alipokuwa akitoka kusikiliza kesi inayomkabili katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mawakili wapinga uhalali mahakama mafisadi kusikiliza kesi ya Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

JOPO la mawakili 14 wanaomtetea Mwenyeki wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na wenzake watatu, wanaomba mahakama iwaachie huru wateja wao kwa sababu Mahakama Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhukumu Uchumi haina mamlaka ya kusikiliza kesi za ugaidi.

Hata hivyo, Jamhuri wamepinga hoja hiyo kwa madai tafsiri si sahihi kwamba mahakama hiyo inayo mamlaka ya kusikiliza shauri hilo. Kutokana na upinzani huo wa hoja, mahakama inatarajia kutoa uamuzi leo wa kama inayo mamlaka au la.

Maombi hayo yaliwasilishwa jana mbele ya Jaji Elinaza Luvanda baada ya Jamhuri kukwama kuwasomea washtakiwa maelezo ya awali kwa sababu upande wa utetezi uliwasilisha pingamizi.

Upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando, Nassoro Katuga, Ignas Mwinuka, Esther Martin na Wakili wa Serikali Tilimanyo Magige.

Upande wa utetezi unawakilishwa na Wakili Peter Kibatala, Jeremiah Mtobesya, John Mallya, Jebra Kambole, Frederick Kihwelo, Sisty Aloyce, Selemani Matauka, Nashon Mkungu, Michael Rugina, Bonifasia Makungu, Alex Maseba, Faraja Mangula, Michael Mwangasa na Gaston Shundu.

Wakili Kidando alidai kuwa kesi ilikuja kwa ajili ya washtakiwa kusomewa maelezo ya awali lakini upande wa utetezi waliwasilisha pingamizi.

Wakili Kibatala alidai ni kweli waliwasilisha pingamizi wakiwa na sababu nne lakini sababu tatu wameziondoa na kubakia na sababu moja ya kwanza inayopinga mahakama hiyo kusikiliza shauri hilo kwa sababu haina mamlaka kisheria ya kufanya hivyo.

"Mahakama hii iko kwa ajili ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, hivyo haina mamlaka ya kusikiliza makosa yaliyofunguliwa chini ya sheria ya kuzuia ugaidi.

"Mashtaka yaliyopo mbele ya mahakama hii yanatakiwa kusikilizwa na Mahakama Kuu ya Tanzania. Hii ni mahakama tofauti kwa sababu ni Divisheni ya Mahakama Kuu na majaji wako maalum kwa makosa ya rushwa na uhujumu uchumi,"alidai Kibatala.

Kibatala aliomba pingamizi likubaliwe, hivyo wanaomba washtakiwa waachiwe huru na mahakama iamuru upande wa Jamhuri kulipa gharama.

Akijibu hoja hiyo, Wakili Kidando alidai hoja za utetezi hazina msingi kwa kuwa tafsiri wanayotoa si sahihi bali ni tafsiri ya zamani kwamba mahakama hiyo ni kwa ajili ya makosa ya rushwa na uhujumu uchumi.

Alidai Mahakama hiyo inayomamlaka ya kusikiliza shauri hilo na hoja iliyowasilishwa ilifanyiwa marekebisho Julai 7, 2016.

Wakili Katuga alidai Bunge ndilo lilisema makosa yote ya ugaidi ni ya uhujumu uchumi na kwamba kutamka si makosa ya uhujumu uchumi ni kupingana na Bunge. Mawakili hao wa Jamhuri waliomba pingamizi litupwe kwa kuwa halina msingi na kwamba mahakama hiyo ina mamlaka ya kusikiliza shauri hilo.

Katuga alidai hoja ya kulipa gharama haina msingi kwa sababu hutokea pale ambapo mahakama inaona Mashtaka dhidi ya washtakiwa yalitungwa.

Jaji Luvanda baada ya kusikiliza hoja zote, alisema mahakama itatoa uamuzi leo asubuhi kama inayo mamlaka au la.

## M'biashara alivyouawa kwa kuchinjwa kichwa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MFANYABIASHARA Elice Patric, maarufu kama Matafu, mkazi wa Kijiji cha Mrimbo Uuwo, Wilaya ya Moshi mkoani Kilimanjaro, ameuawa kikatili na watu wasiojulikana baada ya kuvamia makazi yake na kumchinja shingoni hadi kufa.

Baada ya kutekeleza mauaji hayo yanayotajwa kuwa huenda ni ya kulipiza kisasi, wauaji hao hawakuchukua kitu chochote na kutokomea kusikojulikana.

Akizungumzia tukio hilo jana, Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi, Simon Maigwa, alisema mauaji hayo yanaviashiria vya kisasi.

"Uchunguzi wa awali unaonyesha kuna kulipiza kisasi, lakini kimsingi mpaka sasa tayari tunamshikilia kijana mmoja kwa mahojiano zaidi.

"Marehemu aliuawa kwa kutenganishwa kichwa na kiwiliwili akiwa nyumbani kwake usiku wa jana (juzi), kwa kukatwa shingo. Tunaendelea na uchunguzi wa tukio hilo ili kubaini hasa chanzo cha mauaji hayo."

Diwani wa Mwika Kaskazini (CCM), Samwel Shao, ameliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa tukio hilo.

"Hakuna tukio kama hilo limeshawahi kutokea katika kata yetu, hatujui nini kimetokea, mama huyu ni mfanyabiashara ana watoto watatu na mume. Tumeviachia vyombo vya ulinzi na usalama kuendelea na uchunguzi," alisema Shao.

Baadhi ya majirani akiwamo Rachel Masawe, wakizungumzia tukio hilo, walidai kuwa mfanyabiashara huyo aliuawa kati ya saa 2:00 hadi saa 2:30 usiku, baada ya kutoka katika moja ya eneo lake la biashara na kurejea nyumbani.

"Huyu mama ni mstaarabu, hajui kugombana na mtu, amechinjwa mara alipokuwa ametoka kwenye biashara, wamemtenganisha kichwa na kiwiliwili, inaumiza inasikitisha tunaomba Jeshi la Polisi kuangalia vyema suala hili," alisema Edward Joness.

HABARI KITAIFA



Wanafunzi wa Shule ya Msingi St. Mary's Mbezi jijini Dar es Salaam, Warith Seif na Genesis Msechu wakikata keki kwa ajili ya kuwalisha wazazi kwenye mahafali ya 21 yaliyofanyika shuleni hapo mwishoni mwa wiki na kuhudhuriwa na wazazi na walezi. Nyuma ni viongozi wa shule hiyo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# CAG aja na mbinu ya kuwadhibiti wabadhirifu miradi ya maendeleo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

OFISI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (NAOT), imesema maabara za kiuchunguzi na kiufundi kwenye miradi ya maendeleo zinatarajia kuanza hivi karibuni kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ukaguzi wa mali ya umma.

Aidha, mkandarasi wa maabara ya kiuchunguzi ameshapewa kazi na ameshakamilisha ununuzi na kwamba kuanzia Septemba 13, mwaka huu, ataanza kusimika mitambo, kwa ajili ya kuanza kutumika.

Pia maabara maalum ya ukaguzi wa kiufundi iko katika hatua ya manunuzi na itakamilika kabla ya mwaka huu kwisha.

Akiwasilisha mada mpango mkakati wa miaka mitano wa NAOT na toleo maalum la wananchi la Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2019/20, Mchumi Emmanuel Philipo alisema lengo ni kukagua kitaalamu na kupata ushahidi toshelezi.

Philipo alisema maabara hiyo itakuwa na vifaa malum vya kisasa vya kupima sampo za miradi mbalimbali kama ya barabara na kuondokana na kuchimba sehemu ya barabara au namna nyingine, ili kutafuta ubora unaotakiwa.

"Maabara ya uchunguzi imeshakamilika na tunatarajia itaanza Septemba 13, mwaka huu. Mkandarasi ameshapewa kazi ya kusimika vifaa vya kisasa na ile ya kiufundi," alisema na kuongeza:

"Tunatarajia kuwa hadi mwisho wa mwaka huu maabara zote zitakuwa tayari na zitaanza kutumika, zitaongeza ufanisi kwenye ukaguzi wa miradi ya maendeleo."

Kwa mujibu wa Philipo, CAG yuko katika mchakato wa kuhakikisha kuna ofisi za watumishi wake, ili kuondoa uwezekano wa mkaguzi na mkaguliwa kutumia ofisi moja jambo linalozorotesha uwajibikaji.

Aidha, alitaja aina ya ukaguzi unaofanyika kwa sasa kuwa wa ufanisi ambao wanaangalia thamani ya fedha, wa kiufundi kwa kwenda kwenye miradi na kukagua kwa vifaa maalum kwa kupeleka maabara.

Nyingine ni ukaguzi wa kiuchunguzi, maalum, wa mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) na ukaguzi wa kuzingatia kanuni za sheria au miongozo na sera za shirika, taasisi au ofisi ya umma.

Naye Mkaguzi Paul Shilinde, akiwasilisha mada ya Hati za Ukaguzi, alisema kuna hati nne ambazo ni hati isiyoridhisha, yenye shaka, mbaya na kushindwa kutoa maoni.

Alisema kwa mwaka huo, walishindwa kukagua balozi mbalimbali nje ya nchi kutokana na vikwazo vya kusafiri kutokana na janga la corona na waliishia kukagua Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, jambo ambalo lilisababisha kukosekana kwa ushahidi kutoka kwenye maeneo husika na kutoa hati ya kushindwa kutoa maoni.

# Zitto ataka ukaguzi hesabu za TCD

**Na Gwamaka Alipipi**

MWENYEKITI wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), Zitto Kabwe, amekiomba Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kusaidia kupata mkaguzi wa hesabu atakayefanya ukaguzi maalum wa vitabu vya TCD.

Zitto aliyasema hayo jana, baada ya kikao cha viongozi wakuu wa TCD, ambacho alikiongoza.

Alisema taasisi hiyo haijawahi kukaguliwa hesabu zake tangu mwaka 2016, na kwamba kukaguliwa ni hatua mojawapo ya kuifufua TCD kwa kuhakikisha kuwa fedha za taasisi hiyo zinatunzwa vizuri na kutumika kwa malengo stahiki.

Kutokana na hali hiyo, Zitto aliiomba LHRC isaidie ukaguzi huo katika kipindi cha miezi mwili ijayo.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, alisema taasisi yake imeitikia wito huo na kuahidi kufanyia kazi haraka iwezekanavyo.

"Tumefurahishwa na mwenendo wa kazi za TCD na tuko tayari kuendelea kuwawezesha kwenye suala la kufanya ukaguzi wa vitabu, tutashirikiana kuhakikisha tunalifanyia kazi mapema," alisema Henga.

Kadhalika, Zitto ameanza ziara ya kutembelea wadau muhimu wa demokrasia nchini ikiwamo vyama vya siasa na taasisi za kiraia.

Alipotembelea Taasisi ya Foundation for Civil Society (FCS), viongozi wa taasisi hiyo waliahidi kufanya kazi na TCD katika kuandaa mkutano mkubwa wa haki, amani na maridhiano unaotarajiwa kufanyika mwezi huu.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Legal Services Facility (LSF), Lulu Ng'wanakilala, aliahidi kufanya kazi na TCD katika eneo la nafasi ya wanawake katika uongozi wa vyama vya siasa.

Zitto ameanza ziara ya kutembelea wadau na wanachama wa TCD, baada ya kuteuliwa kuwa mwenyekiti Agosti 26, mwaka huu. Alianza ziara hiyo kwa kutembelea vyama vya waanzilishi wa TCD vya CHADEMA, NCCR-Mageuzi na CUF.




# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Vyama visivyofanya siasa vifutwe sasa

**JUZI** Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ilianza ukaguzi wa vyama vyote vya siasa vyenye usajili wa kudumu kutokana na kuwa takwa la kisheria

Lengo la ukaguzi ni kuhakikisha kuwa vyama hivyo vinakuwa na ofisi katika pande zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa mujibu wa ofisi ya Msajili, pamoja na mambo mengine, mojawapo ya jambo linaloangaliwa kwenye ukaguzi huo ni kukagua ofisi za vyama hivyo Tanzania bara na Zanzibar.

Taarifa ilieleza kuwa ukaguzi na uhakiki wa vyama vya siasa ni takwa la kisheria kuhakikisha vyama vyenye usajili kamili vinatekeleza masharti ya usajili kama yalivyoainishwa kwenye sheria ya vyama vya siasa na kanuni zake.

Hata hivyo, pamoja na Ofisi hiyo kutekeleza takwa hilo la kisheria kwa kufanya ukaguzi na uhakiki wa vyama, baadhi ya wadau wamekuwa wakivilalamikia vyama kadhaa vya siasa kwamba havitekelezi masharti ya usajili, ikiwamo kutokuwa na ofisi zinazoeleweka wala kutofanya shughuli za kisiasa.

Viongozi wa vyama hivyo wamekuwa wakiibuka wakati wa uchaguzi mkuu kuwania udiwani, ubunge na urais, lakini uchaguzi unapoisha hawaonekani tena hadi uchaguzi unaofuata baada ya miaka mitano.

Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 inavitaka vyama kuwa na wanachama pande mbili za Jamhuri ya Muungano, lakini kiuhalisia vyama kadha havitimizi sharti hilo baada ya kusajiliwa.

Msajili wa kwanza wa vyama vya siasa baada ya kurejea kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa, George Liundi, alivifutia usajili vyama vya Tanzania People's Party (TPP) na PONA baada ya kubaini kuwa havikuwa na sifa ya kuendelea kuwapo kutokana na kutofanya shughuli za siasa.

Mrithi wake, John Tendwa, naye hakusita kuvifutia usajili vyama vya CHAUSTA na APPT-Maendeleo, baada ya ukaguzi na uhakiki wa ofisi yake kubaini kuwa vyama hivyo vilishindwa kukidhi masharti ya Sheria ya Vyama vya Siasa Namba 5 ya Julai Mosi, 1992.

Tunatarajia kwamba Msajili wa sasa, Jaji Francis Mutungi, hatakubali kuviacha vyama vya siasa visivyo na sifa kuendelea kuwapo katika daftari lake baada ya ukaguzi kukamilika katikati ya mwezi huu.

Taifa letu linahitaji vyama vya siasa makini na vinavyokubalika kwa jamii kwa kuwa vina mchango mkubwa katika maendeleo na ndivyo vinavyoshika dola baada ya kupata ridhaa ya wananchi.

Tunaishauri Ofisi ya Msajili katika uhakiki wake ijikite pia kuangalia kama vyama vinafanya mikutano yake mikuu ya uchaguzi kwa mujibu wa katiba zao na viongozi halali waliochaguliwa.

Pia rekodi za wanachama wao kama ni hai, ofisi kama ziko kwenye maeneo rasmi na yanayoeleweka ama kwenye nyumba za watu pamoja na mawasiliano rasmi ya kiofisi kati ya chama husika, taasisi zingine na umma kwa ujumla.

Ni matarajio yetu kuona vyama vinavyobabaisha badala ya kuzingatia matakwa ya kisheria na katiba zao vinachukuliwa hatua stahiki, ikiwamo kufutiwa usajili.

Kwa kufanya hivyo, hatutarajii kama kutakuwapo tena na vyama vya ushaguzi ambavyo huibuka tu unapofika mwaka wa uchaguzi na kuitaka serikali ivipatie ruzuku inayotokana na fedha za walipakodi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Christina Mwakangale

## Wanasiasa mnausahau vipi usafi kila mwisho wa mwezi

**ILIKUWA** ni kawaida kuona kila Jumamosi ya mwisho ya mwezi wanasiasa wakijumuika na wananchi kusafisha mitaa, maeneo ya kazi na makazi ya watu mijijini ikiwamo Dar es Salaam.

Hili lilianzia Desema 2015 wakati serikali ilipotangaza kuwa siku hiyo itatumiwa kuhamasisha na kufanya usafi na fedha za sherehe hiyo kuagizwa zielekezwe kwenye ujenzi wa barabara kuanzia Mwenge hadi Morocco jijini Dar es Salaam,

Huo ukawa mwanzo wa viongozi wa mikoa, wilaya na halmashauri kutekeleza hatua za usafi kwenye maeneo mbalimbali na kuhamasisha kila kaya, wafanyabiashara na jamii nzima kuanzia asubuhi hadi saa nne kuutumia muda huu kila Jumamosi ya mwisho wa wiki, kufanya usafi na kusitisha shughuli nyingine.

Hii ilitia moyo. Tofauti na sasa maeneo mengi ya mitaani, barabara, mitaro ya maji taka yamejaa plastiki kama vipande vya matairi, mchanga na unafuu upo kwenye barabara kuu na vituo mabasi ambavyo hufagiliwa.

Barabara kuu mijini zinafanywa usafi kila siku kuondoa mchanga wakati vituo vya mabasi kama Mbezi na Mawasiliano nako usafi unafanyika.

Uzoaji wa taka maeneo na mitaa kadhaa, unasuasua hali ni kama hiyo, hata sokoni na kuliko na mikusanyiko mingi ikiwamo ya wafanyabiashara pembezoni mwa barabara.

Sokoni ambako taka zinazalishwa zaidi kwa mfano taka ngumu hali ni mbaya na iwapo zitapita siku tatu bila taka kuondolewa na mvua ikanyesha eneo lote huchafuka na kukera.

Baadhi ya maeneo ikiwamo Tegeta, Kunduchi, Bunju, Buguruni, Ukonga Mombasa, Temeke na Mbagala kwenye makazi ya watu kunatisha taka zimezagaa haziondolewi na hakuna kufagiliwa, wakazi hawajahamasishwa ipasavyo kushiriki kusafisha maeneo yanayowazunguka na mtindo wa kuishi na takataka umerejea kama zamani.

Wakazi wengi Dar es Salaam kutegemeana na maeneo wanayoishi, hulipia ada ya kuzoa taka katika makazi yao kila kaya ikichangia Shilingi kuanzia 3,000 hadi 10,000 kwa mwezi, ili kugharamia usafi unaofanywa na kampuni binafsi.

Baadhi ya maeneo taka hazibebwi kwa wakati muafaka na kusababisha mlundikano mitaani hali inayozidisha kero ya uchafu, wadudu na wanyama kama panya na mbwa wanaoishi sehemu zilipo, ili kuzitafuna.

Licha ya halmashauri za wilaya na serikali za mitaa kupewa jukumu la kusimamia na kuhakikisha usafi unafanyika, na kazi hiyo kupewa kwa wazabuni, kwa mikataba hata hivyo hakuna mafanikio ya kujivunia.

Hali ikibaki kama ilivyo ni hatari kwa afya za wakazi wa maeneo mengi mijini na mikoani kwa kuwa inawezekana ikiwa chanzo cha magonjwa ya tumbo, kipindupindu na malaria. Kibaya hospitali zinawatibu watu na baada ya kupona wanarudi mtaani kuishi kwenye uchafu na kuendelea kuugua.

Mwaka jana watendaji, wakurugenzi wa halmashauri katika mikoa na wilaya nchini, waliagizwa kuhakikisha usafi na uondoshaji wa taka katika maeneo yao unafanyika kabla ya kuchukuliwa hatua.

Walitakiwa kuvunja mikataba kati yao na kampuni za uzoaji taka, ambazo hazitekelezi majukumu yake na kusababisha ongezeko kubwa la taka mijini, agizo lililotolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira.

Ifahamike kuwa silimia 80 hadi 90 ya taka zinazozalishwa katika majiji nchini hazikusanywi na mamlaka za halmashauri, kwa mujibu wa maelezo ya wizara hiyo.

Halmashauri hasa za miji mikubwa zimeendelea kutoa sababu na visingizio vya mambo yanayokwamisha taka kuondolewa kwa wakati, huku wakikusanya mapato makubwa kutoka kwa wazalishaji wa taka hizo.

Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 kifungu cha 104 na 139 inazitaka mamlaka za miji, majiji na halmashauri za wilaya kuondoa taka, hivyo ni wakati wa kushirikiana na watendaji wa mitaa kuchukua hatua na kuhakikisha usafi unafanyika katika maeneo yao kwa sababu inavyoelekea masuala hayo yanapuuzwa.

## Kamishna Manumba afariki, kuzikwa kesho

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI mstaafu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Kamishna wa Polisi, Robert Manumba (68), alifariki dunia juzi alasiri katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), alikokuwa amelazwa.

Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime, alithibitisha jana kupitia taarifa yake na kueleza kuwa mazishi yanatarajia kufanyika kesho katika kijiji cha Lukungu, wilayani Busega, mkoani Simiyu.

"Tunamkumbuka kama baba, mlezi, mwalimu na kamanda ambaye maofisa, wakaguzi na askari wengi waliopitia katika mikono yake na kujengewa uwezo mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yao ya kulinda maisha ya watu na mali zao," alisema.

Pia alisema watamkumbuka kama mbobezi katika masuala ya upelelezi wa kesi mbalimbali toka ngazi za chini hadi kufikia wadhifa wa juu ndani ya Jeshi la Polisi kwa kuwa DCI.

"Tutamkumbuka kama mtaalamu wa kubuni, kuandaa na kusimamia mikakati mbalimbali ya kubaini, kuzuia na kupambana na uhalifu," alisema.

Kadhalika, alisema Jeshi la Polisi litamkumbuka kama mbobezi wa kujenga uhusiano mzuri na taasisi za ndani na nje ya nchi katika kubadilishana taarifa za uhalifu na wahalifu wa ndani na nje ya nchi.

"Kutokana na ushirikiano huo ulifanikisha kufanya operesheni mbalimbali zenye mafanikio makubwa hasa zilizofanyika kwa kushirikiana na Interpol, nchi za ukanda wa Afrika Mashariki (EAPCCO) na nchi za Ukanda wa Kusini mwa Afrika (SARPCCO)," alisema.

Novemba mwaka 2013, DCI Manumba alistaafu rasmi nafasi hiyo baada ya kufikia umri wa kustaafu kisheria ambao ni miaka 60. Alianza kulitumikia Jeshi la Polisi kuanzia miaka 1975.

Katika utumishi wake ndani ya Jeshi la Polisi, alifanya kazi katika nyadhifa mbalimbali zikiwamo chumba cha kupokea mashtaka kuanzia mwaka (1976 – 1977), mwendesha mashtaka wilaya ya Kibondo na Kasulu mkoani Kigoma (1977 – 1984).

Mkufunzi katika Chuo cha Polisi Dar es Salaam (1984 – 1987), Mkuu wa Upelelezi Wilaya ya Magomeni na Kinondoni na Naibu Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa wa Dar es Salaam (1987 – 1993).

Pia, amewahi kuwa Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa wa Arusha, (1993 – 1995), Mkufunzi Mkuu wa Chuo Cha Polisi Moshi (1995 – 1996), Mkuu wa kitengo cha Fraud makao makuu ya upelelezi (1996 – 1997), Mkuu wa kitengo cha usalama wa nchi, intelijensia na dawa za kulevya makao makuu ya upelelezi (1997 – 2001) na kuwa msaidizi wa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai nchini (2001 – 2006).

Nafasi ya DCI aliishika kuanzia mwaka 2006 hadi anastaafu mwaka 2013.

# Serikali yatoa msimamo kwa waliogushi vyeti

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema haitawarudisha kazini wala kuwalipa malipo yoyote watumishi wote waliobainika kughushi vyeti, Bunge limeambiwa.

Mwaka 2016, serikali ilifanya uhakiki wa watumishi wa umma na kuwaondoa watumishi hewa 19,708 katika daftari na wengine 14,409 walibainika kuwa na vyeti vya kughushi.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, alisema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mikumi (CCM), Dennis Londo.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji watumishi wangapi wamerejeshwa kazini baada ya kuondolewa kimakosa wakati wa uhakiki wa vyeti feki na wafanyakazi hewa.

"Je, ni watumishi wangapi waliorejeshwa kazini wamelipwa stahiki zao kama mishahara ambayo hawakupata kutokana na kuondolewa kimakosa?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Ndejembi alisema utaratibu wa kushughulikia watumishi waliobainika kughushi vyeti ulishatolewa awali na serikali na watumishi wote waliobainika kughushi vyeti hawastahili kurudishwa kazini wala kupata malipo yoyote.

"Napenda kutumia fursa hii kusisitiza kwamba msamaha uliotolewa unawahusu watumishi wale tu walioajiriwa baada ya Mei 20, 2004 bila sifa ya elimu ya kidato cha nne lakini baadaye wakajipatia sifa za kuajiriwa na hauwahusu watumishi waliobainika kuwa na vyeti vya kughushi au waliotoa taarifa za uongo katika kumbukumbu zao rasmi za kiutumishi," alisisitiza.

Pia alisema serikali imewarejesha kazini na kuendelea kuwalipa mishahara watumishi 4,380 walioondolewa kwenye orodha hiyo kimakosa wakati wa uhakiki wa vyeti vya elimu na watumishi hewa.

Aidha, alisema serikali imelipa mishahara ya zaidi ya Sh. bilioni 2.614 kwa watumishi 1,643 kati ya 4,380 waliorejeshwa na inaendelea na uhakiki kwa watumishi waliosalia.

Ndejembi alifafanua kuwa kati ya watumishi 4,380 waliorejeshwa kazini kimakosa, idadi hiyo inajumuisha watendaji wa kata na vijiji na watendaji wa mitaa 3,114.

"Pamoja na kuwarejesha watumishi tajwa, serikali pia ilitoa msamaha wa kuwarejesha kazini watumishi walioondolewa kazini kwa kukosa sifa ya elimu ya kidato cha nne na baadaye wakajiendeleza na kupata sifa tajwa hadi kufikia Desemba, 2020 ambao hawakudanganya katika taarifa zao kuwa wana elimu ya kidato cha nne au kubainika kughushi vyeti."

"Pia, mnamo tarehe 7 Mei, 2021 serikali kupitia ofisi yangu ilitoa maelekezo na utaratibu kwa waajiri kuhusu namna ya kushughulikia hatima za ajira za watumishi walioondolewa kazini kwa kukosa sifa ya elimu ya kidato cha nne pamoja na malipo ya stahili zao," alisema.

# Uyoga wa Tanzania sasa kupata soko Uholanzi



Balozi wa Tanzania nchini Uholanzi, Irene Kasyanju (kulia), akiangalia namna uyoga unavyofungashwa kwenye makasha tayari kwa kupelekwa sokoni huku akipatiwa maelezo ya mchakato mzima wa ufungaji kutoka kwa Mkurugenzi Mwendeshaji wa LIMAX Group, Rob Menheere (kushoto), alipotembelea kampuni hiyo. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NJE**

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI maarufu ya Uholanzi, Limax B.V. (Limax Group) imedhamiria kuwekeza kwenye kilimo cha uyoga nchini kwa kujenga kiwanda cha kusindika na kukausha bidhaa hiyo, mkoani Iringa.

Uwekezaji huo unatarajiwa kuwa na thamani ya Euro milioni 2.1, sawa na Sh. bilioni 5.5 za Tanzania, taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa vyombo vya habari ilibainisha jana.

Hayo yamebainika kutokana na Balozi wa Tanzania nchini Uholanzi, Irene Kasyanju, kutembelea kampuni hiyo Agosti 26, mwaka huu na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi na Mmiliki wa kampuni hiyo, Tom Van Walsem.

Balozi Kasyanju alisema uwekezaji huo utakapokamilika, Tanzania itafaidika kwa kiasi kikubwa kutokana na mtiririko wa biashara ya uyoga kukua kwa kasi duniani.

Kwa mujibu wa Shirika la Chakula na Kilimo (FAO), biashara hiyo inakadiriwa kuongezeka hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 62.2 ifikapo mwaka 2023 kutoka Dola za Marekani bilioni 42.4 mwaka 2018.

Balozi Kasyanju alisema kilimo cha uyoga ni shughuli inayokua kwa kasi nchini Tanzania na thamani yake ya kila mwaka inakadiriwa kuwa Sh. bilioni nne, hivyo ni dhahiri kuwa uwekezaji wa Limax Group utakuwa na tija kubwa na wazalishaji wa uyoga nchini watafaidika na soko kubwa lililopo katika Jumuiya ya Ulaya likiongozwa na Uholanzi ikifuatiwa na Ujerumani na Poland.

Balozi Kasyanju akiwa katika kampuni hiyo alipata fursa ya kujionea mashamba ya kisasa ya uyoga unaozalishwa (si wa asili) na namna zao hilo lenye faida kubwa kwa binadamu linavyosindikwa na kufungashwa.

Kutokana na hatua hiyo, Balozi Kasyanju alielezea matumaini yake kuwa Tanzania itafaidika na uwezo, uzoefu na utaalam mkubwa wa biashara wa kampuni hiyo.

"Tanzania ni nchi yenye maeneo makubwa ya misitu yenye aina anuwai ya uyoga wa porini, kwa ajili ya kula na jamii zimekuwa zinategemea maarifa asilia kukusanya uyoga huo kwa matumizi na kuuza katika masoko ya ndani tu. Ni wakati mwafaka sasa kufanya kazi pamoja kukuza ukuaji wa sekta hii kibiashara," alisema.

# Wahandisi 630 kula kiapo cha taaluma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAHANDISI 630 wanatarajia kula kiapo cha utii wa taaluma yao ili kuhakikisha kuwa wanawajibika vyema katika taaluma zao, uamuzi pamoja na utendaji wao wa kila siku.

Aidha, kiapo hicho kitatumiwa na vyombo mbalimbali kuwawajibisha pale watakapokiuka sheria na taratibu katika majukumu yao ya kila siku.

Mwenyekiti wa kamati ya maandalizi ya mkutano mkuu wa Bodi ya Usajili Wahandisi nchini (ERB) Prof. Bakari Mwinyiwiwa, alibainisha hayo jana jijini hapa wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Wahandisi Tanzania, mwaka huu.

Prof. Mwinyiwiwa alisema maadhimisho hayo yamepangwa kufanyika jijini Dodoma, kwa siku mbili kuanzia kesho katika ukumbi wa Jakaya Kikwete.

Alisema pamoja na mambo mengine katika maadhimisho hayo jumla ya wahandisi 630, watakula kiapo cha utii wa taaluma yao ili kuwafanya wawajibike katika utendaji wa mambo mbalimbali kwenye taaluma yao.

"Bodi ilianzisha utaratibu wa wahandisi wataalamu wote kula kiapo cha utii kwa taaluma yao na kwamba itakuwa ni mwiko kwao kukiuka miiko ya taaluma ya uhandisi," alisema Prof. Mwinyiwiwa.

Pia alisema maudhui ya kiapo hicho yatakuwa ni mhandisi kuanza kuitumikia taaluma kama mtaalamu, kiapo kitamkumbusha jukumu lake kitaalamu na umuhimu wa kuzingatia taaluma wakati wote.

Alifafanua kuwa kiapo kitaufanya umma ujenge imani kwa wahandisi husika, kitatumika dhidi ya mhandisi atakapovunja miiko na maadili ya taaluma katika kumchukulia hatua atakaye kiuka kiapo chake.

"Kiapo kitamlinda mhandisi dhidi ya kulazimishwa kutenda mambo ambayo ni kinyume na taaluma yake, pia kitamkumbusha kuzingatia thamani ya fedha, usalama wa maisha ya binadamu na mazingira, kutoruhusu masuala ya jinai, kidini, jinsia, ukabila, rangi, milengo ya kisiasa katika kutekeleza kazi zake za uhandisi," alisisitiza Prof. Mwinyiwiwa.

# Polisi wenye silaha wadaiwa kuzuia vikao ndani CHADEMA

**Na Thobias Mwanakatwe**

ASKARI Polisi wakiwa na silaha za moto wamezuia kufanyika kwa vikao vya ndani vilivyoitishwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Mkoa wa Mbeya kwenye majimbo ya Kyela na Rungwe.

Vikao hivyo ambavyo vilikuwa na lengo la kuendesha operesheni ya usajili wa wanachama wa CHADEMA kwa kutumia mfumo mpya wa kidijitali, vilizuiliwa juzi kuanzia saa 2:00 asubuhi na jeshi hilo, ambapo baadhi ya askari wakiwa na silaha za moto walifika kwenye kumbi ambako vikao hivyo vilipangwa kufanyika.

Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Mbeya, Joseph Mwasote maarufu 'China wa China' akizungumza na gazeti hili kwa simu akiwa mjini Kyela, alisema kutokana na mfululizo wa Jeshi la Polisi kuendelea kuzuia vikao vyao vya ndani, wanakusudia kufungua kesi ya kikatiba kudai haki.

"Kwa kweli tumechoka kwa unyanyasaji huu tunaofanyiwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, nimeongea na jopo la mawakili tufungue kesi ya kikatiba kudai haki," alisema.

**KAULI YA RPC**

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Urlich Matei, akizungumza na gazeti hili kwa simu akiwa safarini kutoka Dar es Salaam kuelekea Mbeya, alisema hana taarifa za kuzuiliwa vikao vya ndani vya CHADEMA.

Alisema kama kweli CHADEMA wamezuiliwa kufanya vikao vya ndani katika majimbo ya Kyela na Rungwe itakuwa ni kosa kwa kuwa vikao hivyo ni ruhusa kufanyika.

"Navyofahamu vikao vya ndani vya vyama vya siasa vinaruhusiwa, hata CHADEMA walifanya hapa Mbeya Mjini, lakini kama labda wahusika walitaka kulewa mihemko, ambayo inaweza kusababisha kuvunjika kwa amani hapo Jeshi la Polisi lazima liingilie kati," alisema Kamanda Matei.

Mwenyekiti wa CHADEMA akielezea zaidi matukio hayo, alisema polisi wakiwa kwenye magari matatu baadhi wakiwa na silaha za moto walifika katika ukumbi wa Hoteli ya Kasara, mjini Kyela na kuzuia kufanyika kwa kikao hicho cha ndani kwa madai kuwa hawajapewa taarifa kimaandishi kuwapo kwa mkutano huo.

China alisema pia polisi wamezuia mkutano mwingine wa ndani uliokuwa ufanyike jana katika Jimbo la Rungwe ambapo Mkuu wa Polisi wa Wilaya (OCD) alidai wamepewa maagizo kutoka juu kuzia vikao hivyo.

Alisema wanashangazwa na kitendo cha wakuu wa polisi wa wilaya kuzuia vikao hivyo wakati CHADEMA awali walipewa maelekezo ya kumwandikia barua Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa ambaye ni Mkuu wa Mkoa kumjulisha vikao vya ndani, ambavyo vitakuwa vinafanywa na chama hicho.

Alisema utaratibu wa Ma-OCD wa kutaka kila wanapofanya vikao vya ndani wapewe barua kimaandishi unawashangaza, kwa sababu walipewa maelekezo ya kumwandikia barua RC, na kwamba walifanya hivyo.

China alisema barua waliyomwandikia RC wamekuwa wakitembelea nayo, ili kama wakizuiliwa kwenye majimbo wawaonyeshe Ma-OCD, lakini cha kushangaza wanakataa kuitambua na kutaka waandikiwe wao.

Mwenyekiti huyo alisema kitendo kinachofanywa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya kinakwenda kinyume cha maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye hakukataza kufanyika kwa vikao vya ndani vya vyama.



Mratibu wa Mtandao wa Kimataifa wa viongozi wa dini wanaoishi na VVU na walioguswa na VVU/UKIMWI (TANERELA), Mossy Ismail, akizungumza na waandishi wa habari, wakati wa semina ya viongozi wa dini na watu wanaoishi na VVU, kuhusu unyanyapaa na ubaguzi kama kikwazo kwa waathirika, iliyoandaliwa na mtandao huo kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na VVU (NACOPHA), kwa ufadhili wa UNAIDS, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Petroli yateketeza nyumba mbili

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

NYUMBA mbili zenye jumla ya vyumba 17 zilizoko katika kambi ya wavuvi ya Igabiro, Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, mkoani Kagera zimeteketea kwa moto pamoja na mali zote zilizokuwamo katika nyumba hizo, unaodaiwa kutokana na mafuta ya petroli yaliyokuwa yamehifadhiwa ndani nyumba kulipuka.

Akizungumzia tukio hilo, Kaimu Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Wilaya ya Bukoba, Abdulahiman Ngaugia, alisema walipata taarifa za nyumba hizo kuteketea kwa moto juzi saa 11:30 jioni na kuwahi kupunguza madhara kwa kuzima moto huo kabla haujaenea katika nyumba nyingine.

Alisema nyumba zilizoteketea ni mali ya Abduswamadu Kalokola na Frederick Mtoka na kutaja chanzo cha moto huo kuwa ni petroli iliyokuwa ikiuzwa katika nyumba hizo, kwa ajili ya vyombo vya uvuvi na vyombo vingine vya moto.

"Abduswamadu Kalokola ndiye aliyekuwa akiuza petroli na katika nyumba yake kulikuwa na jiko ambalo lilikuwa likitumika kwa shughuli za kupikia na ndilo lilisababisha petroli kulipuka," alisema Ngaugia.

Kufuatia tukio hilo ambalo halikusababisha kifo wala majeruhi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji baada ya kuuzima moto huo, lilitoa elimu kwa wakazi wa eneo hilo na kuwataka kuchukua tahadhari, ili kupunguza ajali za moto.

# Wakulima wafurahia miti mikaratusi kupata soko

**Na Francis Godwin,** IRINGA

BAADHI ya wakulima wa miti katika mikoa ya Iringa na Njombe wameanza kusitisha mpango wa kuteketeza mashamba ya miti ya mikaratusi (milingoti) baada ya soko la miti hiyo kuwa kubwa kutokana na kuanzishwa kwa viwanda vya uchakataji wa nguzo za umeme cha Qwihaya General Enterprises kwenye maeneo yao.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na Nipashe, wakazi hao walisema kuwa miti hiyo kwa muda mrefu ilikuwa ikilimwa kwa matumizi ya kawaida kama kuni na mirunda kwa ajili ya ujenzi, lakini kwa sasa thamani ya miti hiyo imeanza kuwa kubwa baada ya kuwapo kwa viwanda vya nguzo za umeme katika maeneo yao.

Wakazi wa Njombe, Yohana Haule na Evaline Kidenya, walisema kuwa uwapo wa kiwanda cha nguzo za umeme unategemea zaidi miti ya mikaratusi na wao ni wabia wakubwa wa kiwanda hicho.

"Wananchi wengi wa Mkoa wa Njombe kilimo cha mikaratusi tulianza kulima muda mrefu toka enzi za mababu zetu ila hakuna faida kubwa ya miti aina hii zaidi ya kuni na matumizi ya ujenzi, kwa sasa tumeanza kuona mwelekeo wa kunufaika zaidi kwa kilimo hiki."

Festo Sanga na Wilbart Ndelwa, wakazi wa Mufindi mkoani Iringa, walisema zao la miti hiyo kwao limeanza, kuwapa faida kubwa hasa toka kuanzishwa kwa viwanda mbali mbali vya uchakataji wa mazao ya misitu kikiwamo kiwanda cha Qwihaya.

Mkurugenzi wa kampuni za Qwihaya, Leonard Maheda, alisema kampuni zake zinahitaji miti aina ya mikaratusi kwani nguzo wanazotengeneza kwa ajili ya miradi ya umeme nchini na nje ya nchi wanategemea miti aina hiyo.

Aliwataka wananchi kuendelea kulima kwa wingi miti hiyo kwa kuwa soko lake ni kubwa zaidi na endelevu na ukipanda unapovuna inachipua mingine kwa wingi zaidi.

Akielezea kuhusu viwanda mbalimbali alivyoanzisha katika mikoa ya Iringa, Njombe na Kigoma, alisema viwanda hivyo vimeongeza thamani zaidi ya mazao ya miti aina ya mikaratusi pamoja na kusaidia miradi ya maendeleo.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), John Ulanga (wa pili kulia), akimsikiliza Ofisa Mtendaji Mkuu wa SAGCOT, Geoffrey Kirenga (wa tatu kulia), baada ya uzinduzi wa ripoti ya uwekezaji kwa jamii ya SBL, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Naibu Balozi wa Uingereza hapa nchini, Rick Shearn na Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# EABL yaanika uwekezaji wake kwa jamii

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Afrika Mashariki (EABL) imezindua ripoti inayoelezea uwekezaji wake kwa jamii.

Ripoti hiyo ya mwaka 2020 iliyozinduliwa jana, inaelezea kwa undani uwekezaji ambao kampuni hiyo imeufanya kwa jamii katika nchi za Kenya, Uganda na Tanzania ambako inafanya biashara zake.

Kwa Tanzania miradi ya uwekezaji kwa jamii inatekelezwa na kampuni tanzu ya EABL, Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL). Miradi hiyo ni kusaidia upatikanaji wa majisafi na salama, programu ya kilimo biashara inayowasaidia wakulima wazawa, unywaji wa kistaarabu, programu za ujumuifu pamoja na utunzaji wa mazingira kupitia kupanda miti. miradi hiyo inatekelezwa chini ya mpango wa kusaidia jamii unakwenda mpaka mwaka 2030.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa ripoti hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, alielezea baadhi ya miradi inayotekelezwa na kampuni hiyo akianza na miradi ya kusaidia upatikanaji wa majisafi na salama ambapo alisema SBL imeweza kuwafikishia huduma hiyo muhimu Watanzania 2,000,000 ikilenga kurudisha kila tone inalotumia katika uzalishaji wa bidhaa zake. SBL imetekeleza miradi 21 ya maji nchini tangu mwaka 2010.

"Mwaka 2020 tumenunua tani 17,000 za nafaka sawa na asilimia 70 ya mahitaji yetu ya malighafi tunazotumia katika uzalishaji wa bidhaa zetu kwa mwaka ikiwa ni pamoja na shayiri, mahindi na mtama. Katika programu hii inayojulikana kama kilimo biashara, tunafanya kazi na wakulima zaidi ya 400 katika mikoa nane tukiwasaidia kwa kuwapa mafunzo ya kilimo endelevu, huduma za ughani pamoja na kuwaunganisha na taasisi za fedha kwa ajili ya kupata mikopo ya kuongeza uzalishaji wao."

Mradi mwingine ni programu ya kusaidia kuongeza wataalamu wa kilimo kupitia kutoa ufadhili wa masomo maarufu kama kilimo viwanda ambayo imeshawanufaisha wanafunzi 70 wanasomea masomo ya kilimo katika vyuo vinne vya kilimo nchini.

Elimu juu ya unywaji wa kistarabu ni mradi mwingine ambao umekuwa ukitekelezwa na SBL. Mradi huu umeweza kuwafikia maelfu ya Watanzania kupitia kampeni yake ya 'Usinywe na Kuendesha chombo cha Moto'. Kampeni hii inawalenga madereva wa vyombo vya usafiri vya umma, waendesha bodaboda, waenda kwa miguu, wanafunzi wa vyuo na makundi mengine.

Uzinduzi wa ripoti hiyo uliendana sambamba na mjadala juu ya kujenga sekta imara na endelevu ya kilimo ambao uliwaleta pamoja wataalamu kutoka nyanja mbalimbali. Waliohudhuria ni pamoja na mamlaka za udhibiti, wavumbuzi, wafanyabiashara, wakulima, wafanya uamuzi, wachumi na wanadiplomasia.

## Radi yajeruhi 4 Ziwa Victoria

**Richard Makore,** MWANZA

WATU wanne wamejeruhiwa na radi eneo la Sengerema Katunguru katika mwalo wa Kijiweni jijini Mwanza, wakati wakifanya shughuli za uvuvi katika Ziwa Victoria.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Ramadhani Ngh'anzi, alisema watu hao walipigwa na radi katika mwalo huo wakati mvua iliyoambatana na radi ikinyesha na mmoja wao kupokea simu kutoka upande wa pili.

Aliwataja waliojeruhiwa ni Alinus Seneda (39), Jacob John (24), Constantine Rajab (17) na Kusekwa Mahushi (33).

Kamanda Ngh'anzi alisema baada ya tukio hilo majeruhi walikimbizwa katika Hospitali Teule ya Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema (DDH), na hali zao zinaendelea vizuri.

Aidha, alisema kwa mikoa iliyopo Kanda ya Ziwa na Maziwa Makuu inapata athari za matukio ya radi na wataalamu wa hali ya hewa wanatoa tahadhari ya kuzima simu na vyombo vya umeme wakati wa radi.

Alitoa rai kwa watu wanaoishi maeneo hayo kuendelea kuchukua tahadhari ambazo zinatolewa na wataalamu wa hali ya hewa kuepuka athari zinazoweza kutokea.

## Aliyegombea ACT aeleza ya moyoni

**Na Christina Mwakangale**

ALIYEKUWA mgombea ubunge wa Jimbo la Mkuranga, kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Mhandisi Mohamed Mtambo, amesema ataendelea kuwahudumia wananchi katika mazingira yoyote, hata kama hakuchaguliwa kwenye nafasi hiyo.

Mtambo aliyasema hayo kwenye ziara katika Kitongoji cha Chulwi, Kata ya Tambani, Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, akisema mpango mkakati aliokwauandaa, ahadi mbalimbali za kijamii alizozitoa kwa wananchi, ataendelea kuzipatia ufumbuzi kadri inavyowezekana.

Akizungumza na wazee wa mtaa huo, Mtambo alisema uamuzi wake wa kurudi kuwashukuru wananchi waliompigia kura katika uchaguzi mkuu mwaka jana, ni moja ya ahadi zake wakati wa kampeni huku akitoa zawadi mbalimbali kwa wazee hao.

Aliwashukuru kwa ushirikiano waliompatia wakati wote wa kampeni hadi upigaji kura Oktoba, mwaka jana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kumtangaza, Abdallah Ulega (CCM) kuwa mbunge wa jimbo hilo.

"Mwaka jana nilipita hapa kwa wazee wangu kuwaomba ridhaa ili kuwatumikia kama mbunge wa Mkuranga na sababu zangu ni za kizalendo kama kilivyo chama changu cha ACT-Wazalendo. Kwa hiyo sina sababu ya kukata tamaa hata kama nilishindwa.

HABARI BUNGENI

# Upembuzi, usanifu SGR kukamilika mwezi huu

BUNGE limeelezwa upembuzi na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli ya Tabora-Kigoma yenye urefu wa kilomita 411 kwa kiwango cha 'Standard Gauge' unatarajiwa kukamilika mwezi huu.

Hatua hiyo, imetokana na serikali kumwajiri mshauri elekezi kutoka Kampuni ya COWI kwa ajili ya kufanya kazi hiyo.

Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Buhigwe (CCM), Kavejuru Felix.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini serikali itajenga reli ya kisasa kutoka Tabora kwenda Kigoma.

Akijibu swali hilo, Waitara alisema kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) inaendelea na ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha SGR kwa awamu ya kwanza kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza yenye urefu wa kilomita 1,219.

"Kutokana na gharama kubwa za ujenzi na ili kurahisisha ujenzi, awamu ya kwanza inajengwa katika vipande vitano ambavyo ni Dar es Salaam- Morogoro (Km 300), Morogoro-Makutupora (Km 422), Makutupora-Tabora (Km 368), Tabora-Isaka (Km 165) na Isaka-Mwanza (Km 341)," alisema.

Aidha, alisema ujenzi katika vipande vitatu vya Dar es Salaam-Morogoro (Km 300), Morogoro-Makutupora (Km 422) na Mwanza-Isaka (Km 341) unaendelea.

Alibainisha kuwa serikali inakamilisha taratibu za manunuzi ya makandarasi kwa ajili ya ujenzi wa reli ya Standard Gauge kwa vipande vya Makutupora-Tabora (Km 368) na Tabora-Isaka (Km 165).

Kadhalika, alisema serikali inaendelea kutafuta fedha kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo kwa ajili ya kupata mkopo wenye masharti nafuu kwa lengo la kukamilisha ujenzi wa mtandao mzima wa reli kwa kiwango cha Standard Gauge ikiwamo reli ya Tabora-Kigoma (Km 411) na Kaliua-Mpanda- Karema (Km 316.7).



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akijadiliana jambo na Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene (katikati) na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, wakati wa kikao cha Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mikakati 7 ya kuimarisha kilimo yaanikwa

WIZARA ya Kilimo imetaja mikakati saba ya kuimarisha kilimo cha zao la zabibu mkoani Dodoma ikiwamo kuongeza tija ya uzalishaji kutoka tani 6.25 hadi tani 30 kwa hekta ifikapo 2024/25.

Aidha, uzalishaji wa zabibu kwa sasa ni wastani wa tani 16,000 kwa mwaka ikilinganisha na uwezo wa kuzalisha ambao ni wastani wa tani 150,000 kwa mwaka.

Naibu Waziri, Hussein Bashe, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Dodoma Mjini (CCM), Anthony Mavunde.

Katika swali lake, mbunge huyo, alihoji serikali ina mkakati gani wa kuliendeleza zao la zabibu mkoani humo. Akijibu, Bashe alisema katika kuendeleza zao la zabibu serikali imeweka mikakati mbalimbali ikiwamo kuhakikisha upatikanaji wa miche bora kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) na halmashauri za wilaya husika.

Alitaja mikakati mingine ni kuimarisha huduma za ugani katika zao la zabibu, kuongeza upatikanaji wa masoko kutoka asilimia 65 hadi 85, kuweka mazingira bora ya uwekezaji katika tasnia ya zabibu, kufufua na kuanzisha mashamba makubwa ya zabibu na kutenga na kulinda ardhi kwa ajili ya kilimo cha zabibu.

"Serikali imeendelea kuijengea uwezo TARI kuendelea na utafiti na kuzalisha miche kwa kuongeza bajeti ya utafiti wa mazao ya kilimo ikiwamo zao la zabibu kutoka Sh. bilioni 7.35 mwaka 2020/21 hadi Sh. bilioni 11.63 mwaka 2021/22," alisema.

Aidha, alisema serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuwanunulia vitendea kazi maofisa ugani ambao hawana vyombo vya usafiri katika Mkoa wa Dodoma.

"Serikali pia imeweka mkakati wa kufufua mashamba makubwa ya zabibu ambayo uzalishaji wake unasuasua. Katika kutekeleza adhima hiyo serikali imefufua shamba la Chinangali II lenye ukubwa wa ekari 602 lilipo Wilaya ya Chamwino kwa kukarabati bwawa la maji na visima vilivyopo shambani," alisema.

Awali, alisema mahitaji ya mchuzi wa zabibu kwa mwaka ni wastani wa lita milioni 15 ambapo uzalishaji wa ndani ya nchi kwa mwaka ni wastani wa lita milioni tano na kiasi cha wastani wa lita milioni 10 zenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni sita huagizwa kutoka nje ya nchi.

Alisema zabibu ni miongoni mwa mazao ya kimkakati ambayo yamepewa kipaumbele katika kuendelezwa na serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta binafsi na wabia wa maendeleo ili kuongeza uzalishaji na tija kwa wakulima.




# Mchakato waanza kupitia miradi ya Mamlaka za Mitaa

SERIKALI imeanza mchakato wa kupitia miradi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuhakikisha halmashauri za miji, manispaa na majiji inakidhi vigezo na masharti ya matumizi ya hati fungani yatakayoanza mwaka huu wa fedha 2021/22.

Mchakato huo unafanywa kwa kushirikiana na Mfuko wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNCDF) na Mamlaka ya Usimamizi wa Masoko ya Mitaji (CMSA).

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Bahati Ndingo.

Katika swali la mbunge huyo alihoji lini serikali itakamilisha uanzishwaji wa hati fungani za Serikali za Mitaa.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Dugange alisema wakati wa kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2021/22, Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha kuhusu kuanzisha hati fungani za halmashauri.

"Kifungu cha 92 ya hotuba yake ilieleza, katika jitihada za kupanua wigo wa vyanzo vya rasilimali fedha serikali itaangalia uwezekano wa kutumia Hati Fungani zitakazotolewa na Halmashauri za Manispaa na Majiji kama njia mbadala ya kupata rasilimali fedha kwa ajili ya miradi ya kimkakati," alisema.

Alibainisha kuwa hatua hiyo itapunguza mzigo kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali hasa kwa halmashauri zenye miradi ambayo imefanyiwa upembuzi yakinifu na kuwa na uhakika wa uwezo wa miradi hiyo kujiendesha kwa faida.

Hata hivyo, alisema Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura ya 290 Kifungu cha 37 na Kifungu cha 68 vinampa mamlaka waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa kutoa miongozo ya usimamizi wa fedha katika Serikali za Mitaa.

"Hivyo, kwa nyakati tofauti serikali imekuwa ikitoa maelekezo na miongozo kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya halmashauri ikiwamo miongozo ya mikopo na uwekezaji," alisema.

Alisema miongozo hiyo huiwezesha halmashauri kufahamu namna bora ya kubuni miradi ya uwekezaji kwa kuzingatia vipaumbele vilivyotolewa kwa kushirikiana wananchi kwa mustakabali na maendeleo yao.

"Miongozo hii inatolewa na Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI kwa kushirikiana na Waziri mwenye dhamana na Fedha. Hati fungani ni miongoni mwa nyenzo inayotumika kukopa fedha kutoka kwa umma ili kufanikisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo," alisema.

Awali, alisema Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na UNCDF ilianzisha mradi wa majaribio kwa halmashauri nane za manispaa kwa kutoa mafunzo ya ubunifu na uandaaji wa maandiko ya miradi itakayotekelezwa kwa fedha za hati fungani.

Alisema halmashauri nane zilipatiwa mafunzo hayo ikiwamo Halmashauri za Manispaa za Arusha na Mwanza ambazo zilianza maandalizi ya maandiko ya miradi hiyo na kwamba suala hilo lilikuwa la hiari, maandiko hayo hayakukamilika.



Ukurasa 12

Wanasiasa vijana wanavyopania kubadili maisha ya wananchi




Ukurasa 13

Bila kugusa katiba ni ngumu kuboresha sheria za uchaguzi




# siasa

JUMATANO SEPTEMBA 1, 2021

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU






Ukurasa 14

EDGA CHAGWA LUNGU

## Anguko lake lilitazamiwa, aponzwa madeni

KUFUNGA UBALOZI DAR...

# Wanadiplomasia wanaponusa uwezekano athari uwekezaji

**Na Sabato Kasika**

HATUA ya Denmark kutangaza kufunga ubalozi wake nchini, imewaibua wachambuzi wa mambo ya diplomasia wa ndani na nje ya Tanzania wakitoa maoni yao jinsi wanavyoutazama uamuzi huo.

Wachambuzi hao, wakihojiwa na BBC wiki hii wanahofu hatua hiyo inaweza kuwa na athari kwa Tanzania, lakini pia huenda inawezekana Denmark imemaliza malengo yake ya kuwa na ofisi za ubalozi Dar es Salaam na sasa inaondoka.

Mchambuzi Mwangi Maina kutoka Kenya anasema hatua hiyo ina athari za moja kwa moja, kuanzia kwa wawekezaji wa nchi hiyo wanaotaka kuja Tanzania, kwa vile watapata ugumu wa kuja kuwekeza, kwa kuwa hakuna kiunganishi ambacho ni ubalozi wao.

"Iwapo hakuna hali ya taharuki, kufunga ubalozi ni suala la kusikitisha sana, na ukiona ubalozi unafungwa, ujue hawafaidiki na nchi yako ambayo ni Tanzania, kwani biashara ni nipe na mimi nikupe, "anasema mchambuzi huyo akizungumza kwenye kipindi cha Amka na BBC.

Anasema, kwenye diplomasia ya uchumi, watu wanazungumza, wanafanya biashara, lakini inapotokea hali kama hiyo, kunakuwa na changamoto kidogo na kwamba bado nchi hizo zinaweza kukaa na kuzungumza ili ubalozi usifungwe.

"Kwa kuwa serikali ya Tanzania imeonyesha kusikitishwa na uamuzi huo wa Denmark, ninaamini bado kuna uwezekano wa kukaa na kuzungumza kwani bado kuna miaka miwili au mitatu kufikia 2024," anasema.




Waziri Mkuu wa Denmark, Mette Frederiksen, serikali yake itafunga ubalozi Dar. **PICHA: MTANDAO**

Anafafanua kuwa Denmark haiwajibiki kutoa sababu za kuchukua hatua hiyo ya kuamua kufunga ubalozi wake na kwamba jambo la msingi ni nchi hizo mbili kukaa na kuzungumza kwa faida ya serikali na wananchi wao.

"Kuwapo kwa ubalozi, kila upande unafaidika, lakini uhusiano ukizorota, hayo yote yanaondoka, hivyo jambo la msingi ni pande zote kutafuta muafaka, Tanzania imeonyesha kusikitishwa na uamuzi huo, ninaamini itachukua hatua hizo," anasema Mwangi.

**MALENGO YAMETIMIA**

Denmark kutangaza kufunga ubalozi wake nchini, huenda malengo ambayo nchi hiyo ilijiwekea kwa Tanzania, yametimia.

"Huenda nchi hiyo ilikuwa na malengo ya kiuchumi na sasa yametimia na inaamua kufunga ubalozi wake nchini na haiwajibiki kutoa sababu kwa nini imechukua hatua hizo," anasema Godwin Gonde.

Mchambuzi huyu anafafanua kuwa nchi inapokuwa na ubalozi ina lengo fulani na kuwa na ubalozi kuna heshima na faida kubwa za moja kwa moja kwa raia zikiwamo za kufanya shughuli mbalimbali zikiwamo za kiuchumi.

"Lakini kuweka ubalozi katika nchi jirani hakuwezi kuwa na hadhi kama ambavyo ungekuwa ndani ya Tanzania, ndiyo serikali imesikitishwa na uamuzi huo ingawa Denmark imeahidi kuendeleza ushirikiano," anasema.

**KUFUNGA UBALOZI**

Agosti 27 mwaka huu, Waziri wa Mambo ya Nje wa Denmark, Jeppe Kofod, alitangaza kuufunga ubalozi huo ifikapo mwaka 2024, huku sababu zikitajwa kuwa ni kuendana na mpango wa nchi hiyo katika masuala ya kimataifa.

Mbali na Tanzania, nchi hiyo pia itafunga ubalozi wake Argentina, Ubalozi mdogo wa Chongqing nchini China na ujumbe wa biashara huko Barcelona Hispania na inaelezwa kuwa jumla ya uwakilishi 16 na ofisi tisa katika

**INAENDELEA UK.14**

# Wanasiasa vijana wanavyopania kubadili maisha ya wananchi

• Wakusanya mamilioni ya mapato, kuunganisha wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu**

USHIRIKI wa vijana kwenye masuala ya siasa ni suala lisilokwepeka. Ni kwa sababu idadi kubwa ya Watanzania ni vijana. Ndiyo nguvukazi ya taifa, lakini pia ni wapigakura. Ndiyo maana wanahitaji kupata elimu ya uraia na ya mpigakura na mafunzo ya uongozi wahamasike kushiriki siasa.

Wawe wagombea na kushika nafasi mbalimbali za uongozi vijijini na mijini, kwa vile mstakabali wa taifa uko mikononi mwao, anasema Said Malenga, Mwenyekiti wa kitongoji cha Matandu Njenga, kilichoko wilaya ya Kilwa mkoani Lindi, anapozungumzia na Nipashe hivi karibuni.

Anasema amekuwa 'mkitongoji' baada ya kushiriki mafunzo ya uongozi, kilimo hai kinachotumia mbole na viuatilifu asilia yanayolenga kuwezesha vijana kiuchumi, kiuongozi , kupinga rushwa, kujua haki zao, utawala bora, kufuatilia huduma za kijamii na kuwa na jamii zinazojali na kuheshimu usawa wa kijinsia na ushirikishwaji wa wote.

Malenga anasema baada ya kupata mafunzo ya uongozi, mwaka 2019, vijana kutoka vijiji na kata mbalimbali za Wilaya ya Kilwa, walishiriki uchaguzi mkuu wa serikali ya mtaa, vijiji na vitongoji.

Mwanasiasa huyo mwenye miaka 34, anasema mafunzo yaliyotolewa na shirika la ActionAid Kilwa yamewafumbua macho mamia ya vijana wilayani humo, akiwa miongoni mwao, akitokea Kijiji cha Matandu.

"Nilishiriki uchaguzi wa serikali za mitaa kwa tiketi ya CCM na sasa ni Mwenyekiti wa kitongoji cha Matandu Njenga." Anasema na kueleza kuwa anazitambua haki zake za kidemokrasia.

"Kupitia mafunzo hayo vijana wa Kilwa hivi sasa wanajua haki zao, wameanza kushirika katika mikutano mbalimbali ya maendeleo ya vijiji, wanashiriki kwenye uchaguzi wa nafasi mbalimbali za uongozi na pia yamewajengea hamasa ya kuwa viongozi," anasema Malenga.



Mkitongoji Said Malenga, pamoja na siasa, ni mkulima wa matunda anayehamasisha kilimo hai. **PICHA: MWANDISHI WETU**

**USHIRIKI UCHAGUZI 2019**

Baada ya kujua haki za kushiriki uongozi, mwaka 2019 vijana 21 walijitokeza kugombea nafasi mbalimbali kati yao, 15 waligombea nafasi za wenyeviti wa vitongoji, mmoja mwenyekiti wa kijiji na watano ujumbe wa serikali za vijiji, anasema Malenga.

"Vijana sita tulishinda, wawili kati ya 15 walichaguliwa kuwa wenyeviti wa vitongoji, mmoja mwenyekiti wa kijiji na watatu wajumbe wa serikali za vijiji. Kwetu haya ni mafanikio," anasema mwanasiasa huyo.

**ANAJIVUNIA MAFANIKIO**

Malenga anasema kilichowavutia vijana kushiriki katika uchaguzi ni baada ya kujua haki zao, umuhimu na wajibu wa uongozi, kufuatilia uwajibikaji na kufuatilia maendeleo katika maeneo yao.

Malenga ni miongoni wa vijana sita waliochaguliwa kuwa viongozi wa vitongoji na kijiji, anasema mafunzo ya ActionAid Kilwa, yanawafumbua vijana macho, wameshiriki uchaguzi na kuhamasisha wananchi kupigakura na kwamba vijana wakipata mafunzo wanaweza kubadilisha taifa.

> Tofauti na miaka ya nyuma serikali ya kijiji ilikuwa inakusanya kati ya Shilingi milioni mbili hadi tatu kwa mwaka.

Anasema amekuwa chachu ya kuhamasisha vijana na wanawake kupitia mikutano ya vitongoji ili waweze kutumia fedha za mikopo ya halmashauri inayotolewa kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu kuboresha maisha yao.

"Hadi sasa tumeunda vikundi vitatu vya ujasiriamali vijana kipo Hunters Group wajasiriamali wa bodaboda, ambao wamepokea mkopo wa Shilingi milioni 10 na kununua pikipiki nne kutoka fedha za halmashauri na sasa wanafanyabiashara," anasema.

Anataja kingine kuwa ni Tumaini Letu Umoja, hiki ni cha watu wanaoishi na ulemavu wana mradi wa mashine ya kusaga na kukoboa nafaka ambacho kimepata mkopo wa Shilingi milioni sita kutoka Halmashauri ya Kilwa. Anasema mradi huo ulifunguliwa mwezi huu wakati wa mbio za Mwenge na kingine ni cha mama lishe, ambacho kinakamilisha hatua za kuomba mkopo halmashauri.

Malenga anasema anahamasisha kupata huduma za jamii mfano, uhaba wa maji katika kitongoji cha Matandu-Njenga, ameliwasilisha tatizo hilo kwenye Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijni (RUWASA) ili kuwapa wananchi huduma hiyo.

"Juni mwaka huu RUWASA ilikuja kupima sehemu ya kuchimba maji," anasema.

Akizungumzia kilichowashawishi wapiga kura hadi kumchagua kuwa mwenyekiti wa kitongoji ni kutokana na namna alivyotengeneza uaminifu kwa jamii, na ufanyaji kazi ndani ya chama, yote hayo yakichagizwa na mafunzo.

"Kabla ya kuchaguliwa "Nilianzia uongozi ndani ya CCM nilikuwa Katibu wa UVCCM Tawi la Matandu na nikachaguliwa tena kuwa Katibu UVCCM kata ya Kivinje na haya yote ni baada ya kupata mafunzo nikajitambua na kuwajibika kwa ajili ya jamii yangu," anasema.

**WENGINE WAMO**

Ali Choroni mwenye miaka 30, ni zao jingine la mafunzo ya vijana na uongozi, akichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Kiwawa, kilichoko kata ya Mandawa wakati wa uchaguzi wa serikali za mtaa, vijiji na vitongoji 2019.

Anasema uchaguzi huo ulishirikisha wagombea kutoka ACT Wazalendo, CUF na CCM walishiriki akigombea kwa tiketi ya CCM na kupata kura 412 kati ya kura 700 zilizopigwa na kuibuka kidedea.

Anajivunia mafanikio yake kuwa ni pamoja na kukusanya mapato yenye thamani ya Sh. milioni 27, fedha ambazo hazijawahi kupatikana katika Kijiji cha Kiwawa kilichoanzisha mwaka 1964.

"Nimefanikiwa kukusanya fedha hizo katika kipindi cha miaka miwili kutoka kwenye ushuru wa magogo, mbao, mianzi na ufuta. Tofauti na miaka ya nyuma serikali ya kijiji ilikuwa inakusanya kati ya Shilingi milioni mbili hadi tatu kwa mwaka," anasema Chorani.

Anasema ameitisha mikutano ya kijiji kwa mujibu wa sheria kila baada ya miezi mitatu na kusoma mapato na matumizi kwa wanakijiji lakini pia kutunga sheria ndogondogo za mnada wa mazao na pia kutatua matatizo ya wananchi.

Justine Lai ni Mwenyekiti wa Jukwaa la Maendeleo ya Vijana Wilaya ya Kilwa (KIYODI), ambalo ndilo linalishiriki kuandaa vijana hao, anayesema taasisi hiyo inaunganisha vijana takribani 574 wakiwamo wanawake 269 na wanaume 305 ambao wamehamasishwa kupitia mafunzo hayo.

Anasema KIYODI umeundwa kwa kushirikiana na ActionAid na imewaunganisha vijana wa Kilwa kwenye maeneo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ili wajue na kutimiza wajibu wao kwa mujibu wa sera ya vijana ya 2017.

Joyce John, Ofisa Miradi wa ActionAId Kilwa, akizungumzia masuala ya vijana na mafanikio, anasema KIYODI iliyoanzishwa mwaka 2018, inafanya kazi zake katika kata 10 za Kivinje, Singino, Masoko, Miteja, Mandawa, Lihimalyao, Njinjo, Miguluwe, Namayuni, Kipatimo na Mitole.

Anasema wanafanyakazi na vijana kupitia miduara au vikundi vya vijana kwenye maeneo yao na kuhamasisha mambo mengi kama uwajibikaji, ulinzi wa mazingira, uongozi wa kisiasa, uwekezaji na kuondoa umaskini.

# Bila kugusa katiba ni ngumu kuboresha sheria za uchaguzi

**Na Mwandishi Wetu**



Wakili Mlowe katika kazi zake. **PICHA: LAWAGE**

UCHAGUZI ulio huru, haki na unaokubalika unampa kila raia haki ya kushiriki kuchagua viongozi anaowataka kwa kupiga kura ya siri, lakini na yeye kuwa na haki ya kugombea nafasi yeyote ya kuchaguliwa, kutoa maoni na kueleza hisia zake iwapo haridhiki na mwenendo na matokeo ya uchaguzi.

Kurejea sifa hizo na kwa kuangalia hali halisi ya mchakato huo nchini, Rais Samia Suluhu, anaitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kupokea maoni ya wadau na kuzipitia tena sheria za uchaguzi ili kuboresha michakato ya uchaguzi.

Wakili wa kujitegemea Pasience Mlowe wa shirika la Lawage Consult, anazungumza na NIPASHE, kutoa maoni yake kwa NEC wapi pa kuanzia ili kuboreasha uchaguzi...

**SWALI: Wakili, Rais ameelekeza sheria za uchaguzi kupitiwa na wadau kutoa maoni yao ili kuwa na uchaguzi bora, kama mdau, unapendekeza nini kifanyike?**

**JIBU:** Tiba ianze kwenye shina siyo matawi ambayo ni sheria za uchaguzi. Huwezi kutibu matawi ukaacha mzizi mkuu na shina ambayo ni katiba yetu. Ndiyo inayounda NEC, inaipa mamlaka na majukumu.Tatizo ni katiba inayoiunda.

Unapozungumzia kubadilisha sheria za uchaguzi cha kwanza cha kuangaliwa ni katiba. Ibadilike iwe na muundo mpya baada ya hapo tuangalie sheria za uchaguzi zinatoa uhuru wa watu kushiriki? Zinawakwamisha wapi?

Ninaamini tukishamalizana na katiba ni rahisi kupitia na kurekebisha sheria kwa sababu nyingine zimetungwa chini ya katiba ambayo ndiyo sheria kuu. Huwezi kutibu tatizo kwenye sheria za vyama vya siasa na za uchaguzi, kanuni za uchaguzi ambazo zinawanyima fursa Watanzania wengi kushiriki kwa sababu nyingi ikiwamo kuenguliwa kwa kushindwa kuandika majina, bila kugusa katiba.

Kwa hiyo ipo haja Rais atamke sasa bayana "twende kwenye kurekebisha sheria kuu tutengeneze mpya."

Ninasema haya kwasababu, tumepokea ajenda ya kupitia upya sheria za uchaguzi lakini naona kama kuna mkanganyiko. Huwezi kuzungumzia uchaguzi bila kugusa katiba, hiki kipaumbele. Lakini Rais alishasema apewe muda kuimarisha uchumi na katiba isubiri kwanza, naona ni vyema kutafakari na kurejea kwanza kwenye katiba.

**SWALI: Unapendekeza mchakato uanzie wapi?**

**JIBU: Tulishaanza kutengeneza katiba mpya tukashindwa. Hakuna namna ni lazima turudi nyuma katika hatua zote. Tuanze upya ili tuwe na katiba bora inayotupa sheria bora za uchaguzi.**

**SWALI: Kuanza upya ni mchakato kuna kukusanya maoni ya wananchi, bunge la katiba, uchambuzi na kuandaa rasimu, kura za maoni na uidhinishwaji. Unapendekeza kuanza upya wakati kuna nakala mbili ya Warioba na Katiba Pendekezwa ya Bunge, tufanye nini tupata katiba bora?**




**JIBU:** Tukubaliane kuwa tulikwama na sasa ni miaka saba. Tusione kuwa ni jambo gumu. Tukisema twende kwenye kura ya maoni kuchagua ipi bora, bado tutakuwa tunajidanganya. Watanzania wengi watakuwa wamepitwa na mchakato wa 2014 na hawajui tuliishia wapi.

Hivyo, namna ile ile iliyotumika kipindi cha Katiba ya Warioba mchakato ufanyike tena. Kuna mambo yalipendekezwa mwaka 2014 huenda leo hayana uhalisia tena.

Kenya ni mfano walijaribu mara 10 kuandika katiba bila mafanikio lakini wamefanikiwa. Tusikate tamaa. Gharama kubwa inakuja pale wananchi wanapokosa haki yao lakini kama tunaandaa mifumo ya Watanzania kupata haki yao tusijali gharama wala uchumi.

**SWALI: Kwanini unashauri kurejea upya mchakato?**

**JIBU:** Naamini tukisema tuanzie pale tunapoishia tutaacha watu wengi nyuma. Wananchi wanaoweza kujua kilichofanyika ni wale waliokuwa wanafuatilia masuala ya katiba lakini kwa ujumla wengi wakiulizwa katiba mbili hizo zilisema nini hawatakuwa na uelewa sana.

Tuanze upya elimu itolewe, tutoe maoni, yakusanywe na ile hamasa irudi upya, watu wahamasishwe kanisani, misikitini na mitaani ili watoe maoni waseme nini wanachotaka kwenye sheria za uchaguzi na katiba mpya.

Tukumbuke tukiandika katiba mpya tutakuwa na mifumo bora ya uchaguzi ulio huru, haki na unaokubalika, demokrasia pana na tutampunguzia Rais madaraka makubwa, tutakuwa na vyombo na taasisi huru.

Lakini sasa hivi hali ilivyo taifa linategemea sana majukumu yanayotekelezwa na Rais na hili pia ni usumbufu linaweza kumnyima usingizi. Anateua mpaka wakurugenzi wa bodi ana kazi nyingi mno.

**SWALI: Lakini kwa wakati huu, unapendekeza nini katika kuboresha sheria za uchaguzi?**

> Sheria hiyo imetumika hata hivi karibuni kuzuia NCCR-Mageuzi kufanya mkutano wa kamati kuu, kisa haikuomba kibali. Mazingira kama hayo hayawezi kutengeneza vyama imara na makini kushiriki uchaguzi mkuu.

**JIBU:** Ninasimamia kuandika katiba mpya. Lakini kama tutataka tusibadili katiba yote, tuangalie maeneo yenye matatizo mfano kuboresha sehemu ya vipengele vya uchaguzi kama, kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi, uteuzi wa watendaji wake ubadilike. Mgombea huru, matokeo kupingwa mahakamani, vipengele vinavyosema tume ni 'mwanzo na mwisho' kimaamuzi yote haya yaangaliwe.

Leo tunazungumzia masuala ya sheria za uchaguzi, hatuangalii vyama vya siasa vinafanyaje kazi zake. Twende kwenye sheria ya vyama siasa iliyorekebishwa 2019 inayokataza vyama kufanya shughuli za kisiasa kipindi ambacho si cha uchaguzi mfano wakati huu.

Hakuna taifa duniani linaloahirisha shughuli za kisiasa kipindi ambacho si cha uchaguzi ni sawa kusema hakuna vyama vingine vya kisiasa.

Watanzania wanajiuliza hivi kweli chama kipya cha siasa kinachoanza leo wakati ambao hakuna uchaguzi kinapataje wanachama kama hakifanyi mikutano ya kisiasa? Unataka kusema hututaki vyama viongezeke wala visifanye mikutano ya kawaida wala ya uhamasishaji kuungwa mkono na kufahamika?

Sheria hiyo imetumika hata hivi karibuni kuzuia NCCR-Mageuzi kufanya mkutano wa kamati kuu, kisa haikuomba kibali. Mazingira kama hayo hayawezi kutengeneza vyama imara na makini kushiriki uchaguzi mkuu.

Tukumbuke mchakato wa uchaguzi siyo tukio la muda mfupi ni mtiririko wa mambo mengi , uchaguzi mwingine unaanza pale mmoja unapomalizika, vyama lazima vijipange hivyo kuwa na sheria kama hizo ni kuwazuia washiriki kwenye uchaguzi, kadhalika uchaguzi usiwe wa huru na haki. Hivyo katika kuangalia sheria za uchaguzi, sheria kama ya vyama ni lazima kuipitia.

JUKWAA LA VIONGOZI

EDGA CHAGWA LUNGU

# Anguko lake lilitazamiwa, aponzwa madeni

• Kupanda bei za vitu, rushwa kusheheni

**Na Ani Jozeni**

UKIFUATILIA kilichotokea katika anguko la Rais |Edgar Lungu nchini Zambia, akishindwa uchaguzi mkuu na mtu ambaye si mgeni katika siasa za nchi hiyo na ambaye watu wengi wangesema kuwa amechoka, huwezi kukosa vielelezo vya kina kuhusu kilichokosewa.

Ni ule msemo wa Kiswahili kuwa ajidhanie amesimama ajiangalie, asije kuanguka, na inavyoelekea mstaafu Lungu hakutambua kuwa aliposimama kuna walakini, akagundua wakati kura zimeanza kupigwa na kuhesabiwa. Akaashiria kushindwa akidai uchaguzi si huru na wa haki.

**HAKAINDE KAMA LIPUMBA**

Kilihoshangaza wachunguzi wa habari maeneo mengi ni kuwa Rais Hakainde Hichilema, aligombea mara ya sita, ambapo hapa nchini unaweza kumfananisha na Profesa Ibrahim Lipumba wa CUF, kwani hakuna mwingine ameweza kudumu urefu huo katika kinyang'anyiro cha uchaguzi wa rais kila baada ya miaka mitano.

La kushangaza katika hilo ni kuwa mgombea huyo mzoefu sasa ametinga umri wa miaka 59 ambao ingetazamiwa labda ndiyo agombee mara ya pili, kama si ya kwanza. Wapiga kura hawajakimbilia ujana, ni upinzani stadi.

Hata hivyo hali hiyo inamfanya mgombea huo wa mara kadhaa awe mtu maalum kiasi katika siasa za Zambia, kuongoza chama cha upinzani chenye uwezo wa kushinda uchaguzi, ushindwe mara sita na bado chama kikubwa kama hicho kisipate mbadala.

Kwa masuala kama hayo kila nchi na kila uchaguzi unakuwa na majibu yake au kuibua watu wa kushangaza nao wakubalike kwa wapiga kura na hakuna utaalamu kuhusu mazingira hayo. Unachoweza kujadili ni viini vya kutaka chama tawala kitoke madarakani, kumkubali huyo 'veterani' wa kugombea.



Aliyekuwa Rais wa Zambia, Edgar Lungu. **PICHA: MTANDAO**

> Alimshinda Hichilema uchaguzi mkuu 2016 kwa kura chache na alipogombea tena muhula wa pili kamili akashindwa.

Yako maeneo mawili ya kuainisha hapo, hasa kutokana na walichokuwa wanasema wasadizi wake ilipoonekana kuwa kura nyingi za urais zinaelekea kwake.

Wanasema walifaulu kuwatoa vijana wakapige kura, jambo ambalo linasikika katika uchaguzi wa nchi nyingi, hata iwe Marekani kuwa wapiga kura wanapotoka kwa wingi zaidi, na hasa vijana wameanza kushiriki kupiga kura, inakuwa rahisi zaidi mageuzi kufanikiwa. Kimsingi hawana utii wa jadi kwa watawala.

Baadhi ya yale aliyosema Rais Hichilema baada ya kuapishwa hayatofauti na tuliyozoea kusikia kutoka kwa viongozi wa Afrika, ila labda kuna maeneo anaweza kufanya vitu tofauti. Ni suala la mwelekeo wa mabadiliko, ambako kuna ishara kuwa upinzani Afrika unajitahidi kuingia katika masuala ya msingi ya uchumi, na siyo ule upinzani wa jadi wa kupambana na rushwa, ambao kila uchao ulikuwa unaingiza madarakani wala rushwa wengine.

Ni mara ya tatu chama cha upinzani kimechukua madaraka nchini Zambia, na si rahisi kusema kuwa mambo yatabadilika.

Zilikuwepo dalili za wazi kuwa Lungu anaelekea kushindwa, kwani alichukua nafasi ya Rais Michael Sata Januari 2015 alipofariki dunia, na akachaguliwa rasmi 2016 kwa miaka mitano, hivyo ukazuka ubishi kama anaruhusiwa kikatiba kugombea tena.

Alimshinda Hichilema uchaguzi mkuu 2016 kwa kura chache na alipogombea tena kwa muhula wa pili kamili akashindwa, kwani alitumia nguvu nyingi kuzuia upinzani baada ya kuwashinda kwa kura chache. Na hakufaulu kuleta mabadiliko kiuchumi

Licha ya kuwa tatizo kubwa zaidi la vijana nchini Zambia ni kupatikana kazi, kilichomwangusha Lungu ni rushwa, serikali yake ikiandamwa tangu 2018 kuhusu kandarasi za thamani ya dola milioni 284 (zaidi ya Shilingi bilioni 500). Nchi washirika za Finland, Ireland, Sweden na Uingereza zilikata misaada ya dola milioni 34 takriban Sh. bilioni 80, halafu mwaka 2019 yakaja madai ya utakatishaji wa fedha na hata kupitisha fedha kwa vikundi vya kigaidi ukihusishwa na maofisa wa juu wa utawala wa Lungu.

**MADENI**

Inasemekana kuwa nchi hiyo imekumbwa na kushindwa kulipia madeni ambayo muda wake umefika, na jitihada ya Rais Lungu ya kuwahakikishia raia wa Zambia kuwa ataendeleza ujenzi wa miundombinu haikuweza kumsaidia vya kutosha, kutokana na kasi ya mfumuko wa bei.

Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) lilikataa kuikopesha Zambia fedha mwaka 2016 kutokana na serikali hiyo kutokuwa na dhamira ya dhati ya kufanya mabadiliko ya uchumi, taarifa za mashirika ya habari ya kusini mwa Afrika zinaeleza.

Ambacho kitashangaza Watanzania wanaoangalia kurasa za mitandao za viongozi hao wa Zambia, na hata waliowatangulia, ni jinsi wanavyodhihirisha ulokole wa kukata na shoka, kwa mfano Rais Hichilema alifanya ibada ya kwanza ikulu badala ya kwenda kanisani. Mtangulizi wake Lungu ametoa meseji za kuaga katika 'twitter' zenye sura ya mhubiri kanisani, akinukuu mistari kadhaa ya barua za Mtume Paulo kana kwamba yuko kwenye madhabahuni, huku rushwa ikipiga kasi wakati wa utawala wake.

## Wanadiplomasia wanaponusa uwezekano athari uwekezaji

**INATOKA UK.11**

makao makuu ya Wizara ya Mambo ya Nje huko Copenhagen zitaimarishwa.

Katika ufafanuzi wake, waziri huyo anasema, hatua hiyo ni matokeo ya sehemu ya marekebisho ya Denmark ya uwapo wa kimataifa, na kwamba yanajumuisha kuongezeka kwa ujumbe wa kidiplomasia uliopo na kufungwa kwa nyingine.

"Uamuzi wa kufunga Ubalozi Dar es Salaam ni matokeo ya marekebisho ya vipaumbele vya Denmark kwa ushirikiano wa maendeleo kama ilivyoainishwa katika mkakati mpya wa dunia, 'The World we share'," imeeleza taarifa hiyo iliyowekwa katika tovuti ya ubalozi wa nchi hiyo nchini.

Anasema, kutokana na hali hiyo, serikali ya Denmark imeamua kumaliza ushirikiano wa maendeleo baina ya nchi mbili, na kwamba kufunga Ubalozi wa Denmark nchini 2024 na huo haukuwa uamuzi rahisi kufikiwa.

**NI MDAU WA MAENDELEO**

Denmark ni miongoni mwa mataifa wadau muhimu kwa Tanzania, kutokana na kuchangia shughuli mbalimbali za maendeleo kuanzia kwenye ujenzi wa miundombinu ya barabara.

Taarifa mbalimbali zinaonyesha kuwa katika uchangiaji wa miundombinu ya barabara, ilishatoa kiasi cha DKK bilioni 1.9 (takribani Sh bilioni 700, kwenye mchakato wa kuondoa umaskini nchini kuanzia mwaka 2011 hadi 2015 imetoa DKK trilioni 250 , takribani trilioni 91.9.

Nchi hiyo haijaishia hapo tu bali hata kwenye uchaguzi mkuu wa kwanza ndani ya mfumo wa vyama vingi pia imekuwa mdau mkubwa, na imesaidia kuimarisha demokrasia, muundo wa serikali za mitaa imefadhili.

Mbali na hayo, Denmark imechangia kwenye afya ikiwamo kutoa zaidi ya milioni 528 kwa ajili ya kupunguza vifo vya watoto wachanga, wazazi na kupambana na maradhi ya kuambukiza ikiwamo HIV na pia ni mdau mkubwa wa benki moja ikiwa na mamilioni ya hisa.

**MASIKITIKO YA SERIKALI**

Waziri wa Mambo ya Nje, Balozi Liberata Mulamula, anasema hatua hiyo ya Denmark inasikitisha ikizingatiwa kuwa hivi karibuni serikali inafanya jitihada za kufufua na kuimarisha diplomasia na uhusiano wa nchi rafiki ikiwamo Denmark.

"Ni matarajio kuwa Serikali ya Denmark itaendelea kushirikiana na Tanzania kwenye masuala mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kuunga mkono ajenda za Tanzania katika Umoja wa Ulaya, Umoja wa Mataifa na majukwaa mengine ya kimataifa," inaeleza taarifa ya Balozi huyo.

Taarifa hiyo inaeleza kuwa baada ya uamuzi huo wa Denmark, Balozi Mulamula alifanya mazungumzo kwa njia ya mtandao na Waziri wa Ushirikiano wa Maendeleo wa Denmark, Fleming Mortensen.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kulikuwa na jitihada za kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini pamoja na kuimarisha demokrasia na utawala wa sheria na kwamba, walikubaliana na kuendelea kushirikiana na kwamba Mortensen anatarajia kuzulu nchini siku zijazo.





# Mkenda afafanua kuhusu programu kuendeleza kilimo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema inatekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa miaka mitano (FYDP III: 2021/2022-2025/2026) na programu ya kuendeleza sekta ya kilimo awamu ya pili (ASDP II) kwa lengo la kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu wote.

Aidha, wizara ya Kilimo na wizara zingine zinatekeleza sera mbalimbali ambazo zitaiwezesha serikali kufikia malengo iliyojiwekea katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo pamoja na Dira za Maendeleo za Taifa kwa pande zote mbili za Muungano.

Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, alisema hayo jana wakati akizindua ripoti ya sensa ya Kilimo, Mifugo, na Uvuvi ya mwaka wa Kilimo 2019/2020 jijini Dodoma.

Alisema kuwa utekelezaji wa Sera yoyote unahitaji ushahidi wa kisayansi ambao utakuwa macho na masikio ya serikali kupima utekelezaji, tathmini, na ufuatiliaji wa malengo ambayo serikali imejiwekea.

Hata hivyo, Prof. Mkenda alisema takwimu bora zinazokidhi viwango vinavyokubalika ni msingi muhimu wa serikali kujipima katika dhana nzima ya kujenga uchumi shindani na wa viwanda ambayo ni matamanio ya viongozi wote waliopewa dhamana ya kuongoza nchi.

Alisema kuwa mazao ya kilimo yanayozalishwa nchini yanakidhi uhitaji wa chakula cha watu wote Tanzania wapatao takribani milioni 60, kwa asilimia 100.

Waziri huyo alisema uzalishaji wa mazao pia unatoa ziada kwa ajili ya kuuza nje na kulipatia taifa fedha za kigeni.

Alieleza kuwa shughuli za kilimo ambazo zinajumuisha mazao, mifugo, misitu na uvuvi zimeendelea kutoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa kujenga uchumi shindani na wa viwanda.

Aidha, shughuli hizi za uchumi zimeendelea kutoa ajira kwa zaidi ya asilimia 65, ya Watanzania wote wenye uwezo wa kufanya kazi hususani kwa wale wanaoishi katika maeneo ya vijijini na wengi wao wakiwa wanawake na vijana.

Awali akizungumza katika hafla hiyo Mtwakimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema kuwa sensa hiyo ni ya tano na kabla yake zilifanyika sensa nne yaani mwaka 1971/72; 1993/94 na 1994/95, 2002/03 na ya nne ni ya mwaka 2007/08.

Alifafanua kuwa Tanzania imekuwa ikiendesha sensa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kila baada ya takribani miaka 10. takwimu za uchumi zilizopo zinaonesha mchango wa shughuli za kilimo katika Pato la Taifa umeongezeka hadi asilimia 26.9 mwaka 2020 ikilinganishwa na asilimia 26.6 mwaka 2019.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi za sekta hii ambazo zinajumuisha kilimo cha mazao, mifugo, misitu na uvuvi zilikua kwa asilimia 4.9 mwaka 2020, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.4 mwaka 2019.

Kwa upande wake mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, alisema uzinduzi huo umekuja wakati muafaka kwani itasaidia wizara na taasisi mbalimbali katika kuongeza tija na uzalishaji wa mazao mbalimbali nchini.

# Wabunifu, wagunduzi 1,785 waibuliwa ndani ya miaka 3

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNIFU na wagunduzi wa teknolojia mbalimbali zinazozalishwa nchini 1,785 wameibuliwa ndani ya miaka mitatu ya Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU).

Aidha, Serikali imepanga kutumia Sh. bilioni 43 kwa ajili ya kuanzisha vituo atamizi kwa ajili ya kuendeleza teknolojia na ubunifu katika taasisi na vyuo vikuu nchini kupitia mradi wa Elimu ya Juu kwa ajili ya mapinduzi ya Kiuchumi (HEET) unaoanza mwaka huu 2021/22.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua kikao kazi cha Maofisa Maendeleo ya Jamii kwenye Halmashauri nchini kuhusu masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

Alisema kuna wabunifu mahiri 130 wanaendelezwa na Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), ili ubunifu wao uweze kufikia hatua ya kubiasharishwa, hivyo kuongeza kipato na fursa za ajira kwa vijana.

Kadhalika, alisema Wizara kwa kushirikiana na ofisi za makatibu tawala wa mikoa, imetambua na kuhakiki teknolojia zilizozalishwa na vijana wa Kitanzania 389 na taarifa zake kuingizwa kwenye kanzidata ya wizara inayohusu utafiti na ubunifu.

Akizungumzia kuhusu mradi wa HEET, alisema unatekelezwa kwa fedha kutoka Benki ya Dunia na kubainisha kuwa serikali imedhamiria kuhakikisha ubunifu unapewa kipaumbele cha hali ya juu katika kuharakisha maendeleo kijamii na kiuchumi.

Alitaja vituo vitakavyoanzishwa ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, Taasisi ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia, Chuo Kikuu Mzumbe, Chuo Kikuu Ardhi, Chuo Kikuu Huria Tanzania na COSTECH.

Aliziagiza taasisi zinazohusika na masuala ya teknolojia na ubunifu nchini kuongeza kasi ya kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu wachanga na kuwajengea uwezo stahiki ili kuhakikisha bunifu zao zinalindwa ipasavyo.

"Natoa wito kwa wabunifu kuendelea kujitokeza ili ubunifu wao utambuliwe na kuendelezwa kupitia vituo hivyo," alisema.

Hata hivyo, alisema wizara imeandaa kikao hicho kutokana na uwapo wa baadhi ya vikwazo vilivyojitokeza wakati wa ukusanyaji na uhakiki wa taarifa za teknolojia na bunifu zilizotambuliwa.

"Changamoto hizo ni ukusanyaji hafifu wa taarifa za wabunifu kutoka ngazi za Wilaya, Kata, Vijiji na Mitaa na mwitikio hafifu wa baadhi ya wabunifu katika zoezi la utambuzi teknolojia na ubunifu na hata kushiriki kutokana na uelewa mdogo kuhusu dhana nzima ya teknolojia na ubunifu na umuhimu wa kutoa taarifa sahihi za wabunifu hao," alisema.

Alisema maofisa hao baada ya kikao watashiriki kikamilifu katika kuwaibua, kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu wachanga hasa wale wanaotoka katika mfumo usio rasmi.

Awali, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. James Mdoe, alisema ushirikiano huo utasaidia kuwaibua wabunifu wa ngazi ya chini na kuchangia kikamilifu kwenye pato la taifa.



Mkazi wa Mtaa wa Ndachi B Centre Block D, jijini Dodoma, Said Salum akiwa na familia yake nje ya nyumba yake waliyokuwa wakiishi toka mwaka 2004, baada ya kuvunjwa na Halmashauri ya Jiji hilo, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Bil. 1.3/- kukamilisha mradi wa maji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amesema Sh. bilioni 1.3 zimetolewa na serikali kukamilisha mradi wa maji kwa wakazi wa Njendengwa, Ihumwa, Nzuguni, Nyumba mia tatu, Iyumbu, soko kuu la Ndugai na FFU jijini Dodoma.

Aweso aliyasema hayo juzi alipofanya ziara ya kutembelea maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa maji wa Ihumwa Njedengwa wenye thamani ya Sh. bilioni 2.7 unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Dodoma (DUWASA).

Waziri huyo alisema Rais Samia Suluhu Hassan ametoa fedha hizo kwa ajili ya kukamilisha mradi huo kwa kufanya ununuzi wa vifaa na usimikaji wa pampu kubwa mbili za kusukuma maji.

"Fedha hizi ni kwa ajili ya ulazaji wa mabomba ya kupeleka maji kwenye tangi lenye urefu wa KM11.6, ulazaji wa mabomba ya kusambazia maji yenye urefu wa Km 5.6 kwenda maeneo ya Iyumbu, Njedengwa na Mwangaza, Nyumba 300, FFU, Standi Kuu ya mabasi, Soko la Job Ndugai na eneo la Nzuguni," alisema.

Waziri Aweso aliitaka DUWASA kuongeza nguvu mara watakapopata fedha hizo ili kazi ikamilike ndani ya miezi miwili kuanzia sasa na wananchi waanze kupata maji. Alifafanua kuwa awali serikali ilitoa Sh. bilioni 1.4 kwa lengo la kufanya makao makuu ya nchi Dodoma kuondokana na changamoto ya majisafi ambayo ilikuwa ikiwakabili wananchi.

"Tunajua serikali inayoongozwa na Mama yetu mpendwa Samia Suluhu Hassan ni serikali ambayo inawajali wananchi wa hali ya chini. Pamoja na kuwajali watu wa hali ya chini, inakusudia kumtua mama ndoo kichwani."

"Kwa maana hiyo, Mama yetu Samia ameona ni vyema kuwawezesha wakazi wa Dodoma ambako ni makao makuu ya nchi, Sh. bilioni 2.7 kwa ajili ya usambazaji wa maji katika maeneo haya," alisema

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA, Mhandisi Aron Joseph, alisema mradi huo pamoja na kuwa umefikia hatua nzuri lakini changamoto ni kuwepo kwa miamba wakati wa uchimbaji wa mitaro ya utandazaji wa mabomba.

Alisema, watatekeleza maagizo ya Waziri Aweso ili kuhakikisha adhima ya serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan ya kumtua ndoo mama kichwani inafikiwa.





# Chunya wamlilia kijana Hamza

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SIKU chache baada ya kijana Hamza Hassan (30) kufariki dunia kwenye majibizano ya risasi na polisi mkoani Dar es Salaam, wakazi wa Kijiji cha Mwanzo Mgumu katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makongolosi wilayani Chunya alikokuwa amewekeza migodi ya dhahabu, wamesema kifo chake kimeacha pigo kwao.

Nipashe ilifika katika eneo la mgodi wa Kwa Msomali ulioko katika kijiji hicho ambao ulikuwa unamilikiwa na Hamza na kukuta shughuli za uchimbaji zikiwa zimesimama huku akiwa amebaki kijana mmoja pekee ambaye analinda vifaa.

Wananchi wa kijiji hicho walidai kuwa tukio alilolifanya Hamza la kuua askari na baadaye kuuawa liliwashtua kutokana na historia yake kuwa nzuri tangu walipoanza kuishi naye akiwa mdogo.

Walisema alikuwa msaada mkubwa kwao kutokana na kuwasaidia kujenga baadhi ya miundombinu na kuwaahidi kuwasaidia zaidi kujenga na mingine ambayo walikuwa wanahitaji kijijini hapo ikiwamo ujenzi wa shule.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa kijiji hicho, Eva Said, alisema kijana huyo aliwasaidia kujenga ofisi ya chama tawi la Mwanzo Mgumu kuanzia hatua ya awali mpaka kuikamilisha na akawaahidi kuwanunulia na viti kwa ajili ya ofisi hiyo.

Alisema kijana huyo alikuwa mchapakazi na ni miongoni mwa wawekezaji waliosaidia kijiji chao kupata maendeleo, hivyo kifo chake kimeacha pengo kubwa kwenye maisha yao.

"Tumeishi na Hamza kwenye kijiji chetu kwa miaka mingi. Hakuwahi kufanya tukio lolote baya. Yeye ndiye aliyetusaidia kujenga ofisi yetu hii maana alisema anataka kukiendeleza kijiji chetu. Kwa hiyo ametuachia pigo ambalo ni la ghafla mno," alisema Said.

Naye Upendo Mwashiuya alisema kijana huyo aliahidi angewasaidia kujenga shule ili kuwapunguzia watoto wa kijiji hicho umbali wa kwenda shuleni katika vijiji jirani, hivyo kifo chake kimesababisha ndoto za kuwa na shule kuanza kufifia.

Alisema siku ya kwanza wakati wanapata taarifa kwamba kijana huyo amefariki dunia, walidhani pengine alipata ajali lakini baadaye wakaambiwa alikuwa anawashambulia askari kwa risasi jambo ambalo liliwashtua zaidi kutokana na tabia zake.

Baadhi ya vijana waliokuwa wanafanya kazi kwenye mgodi wa kijana huyo, walisema baada ya kusikia kifo cha mwajiri wao, matumaini ya ajira yao kuendelea yamefifia na mpaka sasa hawana uhakika kama wataendelea kufanya kazi kwenye mgodi huo ama ndio mwisho wao.

Mmoja wa vijana hao, John Mteru, alisema alianza kufanya kazi mwaka jana ambapo aliajiriwa kwenye mgodi kama mchimbaji na tangu wakati huo hakuwahi kukorofishana na bosi wake wala hakuwahi kuona akigombana na mtu yeyote.

Alisema tukio lililotokea lilikuwa sio la kawaida na kwamba tangu alipoanza kufanya kazi kwenye mgodi huo hakuwahi kujua kwamba Hamza alikuwa anamiliki silaha ya moto.

"Aliondoka hapa Agosti 9, mwaka huu, na aliaga kwamba anaenda Dar es Salaam japo hakusema anaenda kufanya nini na atarudi lini. Sasa tulipopata taarifa za kifo chake tulichanganyikiwa na wengine waliondoka tumebaki wachache sana na hatuna uhakika kama ajira yetu," alisema Mteru.

Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Wilaya ya Chunya, George Mtasha, alisema anamfahamu kijana huyo kabla baba yake, Mzee Hassan, hajafariki dunia na kwamba alikuwa anaenda mara moja moja kumsalimia baba yake.

Alisema kijana huyo alikuwa anafanya kazi kwa kujituma na kwamba ni miongoni mwa vijana ambao wamesimamia mali za urithi kwa mafanikio akishirikiana na kaka yake aitwaye Yusuph.

Alisema chama hicho kinaendelea kufuatilia taarifa zaidi kutoka kwa wanafamilia pamoja na Jeshi la Polisi ili kujua chanzo halisi cha kijana huyo kufanya tukio la mauaji ambalo sio la kawaida.



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani akifungua maji kutoka kwenye kisima kilichochorongwa kwa ajili ya kuzalisha umeme utokanao na jotoardhi katika eneo la Mbaka Kyejo, Halmashauri ya Busokelo, wilayani Rungwe, mkoani Mbeya alipofanya ziara ya kukagua mradi huo hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mgogoro KKKT wagawa waumini

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

MGOGORO wa kuhamisha Makao Makuu ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Konde kutoka Tukuyu wilayani Rungwe kwenda jijini Mbeya, umeendelea kuwagawa waumini baada ya waumini wa kanisa hilo Jimbo la Kusini kuandaa waraka wa kuunga mkono kuhamishwa kwa dayosisi hiyo.

Aidha waumini hao walifanya ibada maalumu ya kuliombea kanisa hilo ili mgogoro huo ufike mwisho na kazi ya kueneza injili iendelee huku wakiwataka wenzao wa maeneo mengine kuwaunga mkono.

Wakizungumza kwenye kikao maalumu kilichofanyika katika ukumbi wa kanisa hilo uliopo Matema wilayani Kyela, waumini wa Jimbo la Kusini lenye makao makuu yake Kyela, walisema hakuna tatizo lolote makao makuu ya dayosisi hiyo kuhamishwa.

Akisoma waraka wa waumini hao, Edger Mwakasangule, alisema mgogoro unaoendelea ndani ya kanisa hilo ni udhalilishaji wa kanisa, hivyo hawaoni sababu ya kupinga kuhamishwa kwa makao makuu ya dayosisi.

Alisema wanachotaka ni kuendelea kumcha Mungu bila kujali makao makuu ya Dayosisi yako sehemu gani na kwamba ndiyo sababu ya wao kutopinga kuhamishwa kwa dayosisi kutoka Tukuyu kwenda Mbeya Mjini.

"Hatuoni sababu yoyote ya kupinga kuhamishwa kwa dayosisi hii. Tunawaomba wenzetu wanaopinga waachane na jambo hili maana linatia doa kwenye kanisa," alisema Mwakasangule.

Alisema uamuzi wa kuhamisha makao makuu ya Dayosisi hiyo uliamuliwa na Mkutano Mkuu wa Dayosisi ambao ni chombo chenye mamlaka kwa mujibu wa katiba ya dayosisi hiyo.

Mchungaji Mstaafu Isakwisa Mwaijumba alisema wastaafu hawapaswi kuingilia mgogoro badala yake wanabaki kuwa washauri wa kulisaidia kanisa ili lienende katika njia sahihi.

# Utafiti wabaini fursa kilimo cha kakao, chikichi Rukwa

**Na Nebart Msokwa,** SUMBAWANGA

MKOA wa Rukwa umebainika kuwa na udongo unaofaa kwa kilimo cha kakao, chikichi na karanga pori maarufu makademia, ambayo hayajawahi kulimwa ndani ya mkoa huo.

Utafiti ambao umefanywa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Kituo cha Uyole umeonyesha kuwa mazao hayo yanaweza kuzalishwa vizuri ndani ya mkoa huo na kusaidia nchi kuondokana na uhaba wa mafuta ya kupikia pamoja na kuinua kipato cha wananchi wa mkoa huo na taifa kwa ujumla.

Akitoa taarifa ya utafiti na upimaji wa afya ya udongo mkoani Rukwa, Mkurugenzi TARI Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema kazi hiyo imeonyesha uwapo wa tatizo la tindikali kwenye udongo katika baadhi ya maeneo ya mkoa, lakini wamegundua mkoa una uwezo wa kulima mazao mengine ya biashara.

"Katika utafiti tulioufanya, tumebaini baadhi ya maeneo ya mkoa wa Rukwa udongo wake una tatizo la tindikali, lakini kuna faida ambazo tumezigundua ikiwamo mazao mapya ambayo yanaweza kulimwa kwa tija ndani ya mkoa huu na wananchi wakanufaika," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisema mazao ya chikichi, kakao na karanga pori yanaweza kustawi katika maeneo ya mwambao wa Ziwa Rukwa na Ziwa Tanganyika mkoani Rukwa bila shida yoyote.

Dk. Bucheyeki alisema mbali na faida hiyo, upimaji wa afya ya udongo pia una faida zingine nyingi ikiwamo kuwapatia wakulima ushauri sahihi wa mbolea wanazostahili kutumia kulingana na mazao wanayolima na kuwaelekeza namna bora ya kuzalisha mazao kwa tija.

Alisema tayari wataalamu wa kilimo wapatao 34 tayari wamepewa mafunzo maalum ya namna ya kutambua matatizo ya udongo yanayoweza kuathiri mazao ya wakulima na namna ya kukabiliana nayo.

Mtafiti wa Udongo kutoka TARI Uyole, Fredrick Mlowe, alisema baada ya kubaini uwapo wa tindikali kwenye udongo katika baadhi ya maeneo ya mkoa wa Rukwa, tayari wameshapendekeza mbinu za kukabiliana na tatizo hilo.

Miongoni mwa mapendekezo hayo, alisema ni matumizi ya chokaa kwenye udongo kwa ajili ya kudhibiti tindikali na kwamba tayari wameshawasiliana na kiwanda cha chokaa kilichoko Dodoma kwa ajili ya kuwapatia wakazi mkoa wa Rukwa chokaa ya kuweka mashambani ili kukabiliana na tatizo hilo.

Utafiti na upimaji wa afya ya udongo vinalenga kufanyika katika mikoa ya Morogoro, Mbeya, Iringa na Rukwa na linafanywa kwa ufadhili wa Kampuni ya OCP kwa niaba ya serikali.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya OCP, Dk. Mshindo Msola, alisema lengo la utafiti huo ni kujua matatizo yaliyopo kwenye udongo na yanayosababisha uzalishaji wa mazao nchini usifanyike kwa tija.

Alisema kazi hiyo kwa sasa ni lazima ifanyike nchi nzima kwa ajili ya kuwahakikishia wananchi kilimo chenye tija sambamba na kuinua kipato chao na taifa kwa ujumla.

"Utafiti huu ni muhimu sana na kwa kweli ni lazima ufanyike kwa sababu tunahitaji kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kwa manufaa ya taifa letu," alisema Dk. Msolla.



## RC abainisha kupungua kwa siasa za chuki

**Na Rahma Suleiman,** PEMBA

MKUU wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Samala Mbarouk Kharib, amesema wananchi wameondokana na siasa za chuki na uhasama ambazo awali ziliota mizizi.

Aliyasema hayo jana katika ukumbi wa Halmashauri ya Micheweni wakati akiwasilisha ripoti ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo mbele ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi. wakati wa ziara yake katika mkoa huo.

Samala alisema hali ya amani na utulivu katika mkoa huo inazidi kuimarika kutokana na uwapo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK).

Alisema maendeleo yaliyofikiwa katika mkoa huo yanatokana na ushirikiano mkubwa uliopo kati ya serikali ya mkoa, Chama Cha Mapinduzi na vyama vingine vya siasa kikiwamo ACT-Wazalendo.

Mkuu huyo wa mkoa alisema wananchi wa mkoa huo unategemea zaidi kilimo hasa karafuu na mwani, uvuvi, ufugaji, ujasiriamali, biashara na mazao ya viungo.

Alisema changamoto inayowakabili wakulima wa mkoa huo ni mabadiliko ya tabia nchi inayosababisha uvamizi wa maji ya bahari katika maeneo ya kilimo na uhaba wa wataalamu wa kilimo.

Kwa mujibu wa Samala, mkoa umechukua hatua ya upatikanaji wa wataalamu na kuendelea kuwashauri wakulima kushiriki kujenga matuta ya kuzuia maji chumvi ikiwa ndiyo njia pekee ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi katika mabonde 12 kwenye mkoa huo.

Alisema wakulima wa mwani wanaendelea na shughuli za upandaji wa zao hilo na kuiomba serikali kuharakisha ujenzi wa kiwanda cha mwani ili kuongeza thamani na bei.

Kuhusu udhalilishaji wa kijinsia, Mkuu wa Mkoa huyo alisema kesi 74 za udhalilishaji zimeripotiwa katika vituo vya polisi ikiwamo kubaka 39, kutorosha 10, kulawiti sita, shambulio la aibu 16 na kunajisi watu watatu wenye ulemavu wa akili.

Alisema kesi 13 ziko mahakamani, kesi tisa zimefungwa na Ofisi ya Mkurugenzi wa mashtaka DPP, kesi moja iko kwa DPP na kesi 51 ziko polisi kwa upelelezi.

Hata hivyo, alisema changamoto kubwa iliyojitokeza wananchi hawafiki mahakamani kutoa ushahidi kutokana na muhali.

Alisema mafanikio yaliopatikana ni asilimia 80 za kesi wametiwa hatiani kwa kutoa ushahidi na asilimia 20 ni wasiofika mahakamani na walioachiliwa kwa sababu mbalimbali.

# Wafurahia manufaa tamasha la Kizimkazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJASIRIAMALI wa Mkoa wa Kusini Unguja wamesema tamasha la Kizimkazi limeleta manufaa kwao kwa sababu lilikuwa soko la uhakika wa kuuza bidhaa zao.

Akizungumza na Nipashe, Sinajambo Mkonde Makame, mjasiriamali anayetengeneza mikoba ya ukili, alisema biashara yake ilikuwa nzuri wakati wa maonyesho hayo kwa sababu mikoba yote 10 aliyochukua ilinunuliwa.

Sinajambo alisema wajasiriamali wanakabiliwa na tatizo la soko, hivyo matamasha kama hayo huwa fursa kwao kuuza bidhaa zao.

"'Nashukuru mikoba yangu yote nimeuza, nimekuja na mikoba 10 na mkoba mmoja nauza Sh. 30,000 na yote imetoka," alisema.

Mjasiriamali huyo aliomba serikali kuandaa na matamasha ya mara kwa mara ili kupata fursa ya kutangaza na kuuza bidhaa zao.

Alisema licha ya tatizo la soko kwa ajili ya kuuza bidhaa zao pia kuna changamoto ya upatikanaji wa ukindu kwa ajili ya kutengenezea mikoba.

Naye Futari Ali Abdallah kutoka kijiji cha Kizimkazi, alisema maonyesho hayo ni faraja kwao wameuza bidhaa zao ambazo zimesaidia kupata kipato.

Futari, mjasiriamali anayetengeneza vinyago, alisema bidhaa zao huuza zaidi katika hoteli za kitalii na ni mara yake ya kwanza kuuza katika maonyesho ya tamasha na kwamba wateja wengi wamevutiwa na bidhaa zake.

"Soko langu zaidi lipo katika hoteli za kitalii lakini nashukuru baada ya kuja na bidhaa zangu katika tamasha hili nimeuza vizuri," alisema.

Akizungumza katika tamasha la Kizimkazi wakati Rais Samia alipotembelea maonyesho hayo, Mwakilishi Hamida Juma, alisema Benki ya CRDB ilitoa mafunzo ya elimu ya kuweka hakiba kwa wajasiriamali 450 wa mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema lengo la mafunzo hayo kutatua changamoto ya soko kwa wajasiriamali na kuyatumia matamasha mbalimbali katika kutangaza bidhaa zao.




Mfugaji wa nyuki katika kijiji cha Pujini Pemba, Abdallah Salum Issa, akizungumza na Nipashe, wakati wa mahojiano kuhusu ufugaji wa nyuki jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Chanzo kupungua uzalishaji asali chatajwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAFUGAJI wa nyuki Zanzibar wamesema uzalishaji wa asali umepungua kutokana na sababu mbalimbali.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, walisema uzalishaji wa asali umepungua kwa sababu ya nyuki kukosa maua.

Abdallah Salum Issa, mfugaji wa nyuki katika Kijiji cha Pujini Pemba, alisema soko la asali ni zuri sana lakini kiwango cha upatikanaji kimepungua.

Alisema walikuwa wakivuna lita 20 za asali kwa mzinga mmoja wa nyuki, lakini hivi sasa uzalishaji umepungua kutokana na wadudu waharibifu wanaowashambulia nyuki, hivyo kusababisha nyuki hukimbia.

Kwa mujibu wa mfugaji huyo, lita moja ya asali ya Pemba inauzwa Sh. 40,000 na soko ni zuri sana lakini kiwango cha upatikanaji wa asali kimepungua.

Alisema kiwango hicho ya asali kimepungua kwa sababu wakulima wa matunda na mboga kutumia dawa za kemikali kwa ajili ya kilimo hicho, hivyo nyuki hushindwa kupata chakula katika maua ya mimea hiyo ikiwamo maua ya nyanya.

"Utumiaji wa dawa zenye kemikali kwa wakulima umetuathiri sana sisi wafugaji wa nyuki kwa sababu nyuki hushindwa kupata chakula katika mimea hiyo ambayo hutoa maua," alisema.

Alisema ukataji wa miti nao pia unachangia uzalishaji wa asali kupungua kutokana na nyuki kuhama sehemu moja na kwenda nyingine, hivyo eneo ambalo lilikatwa miti hushindwa kupata asali.

Rajab Suleiman Khamis kutoka Kijiji cha Kitogani, Unguja, alisema pia wanakabiliwa na wizi wa asali katika mashamba yao hali ambayo inawarejesha nyuma kimaendeleo katika shughuli hiyo.

Alisema pia Zanzibar hakuna maduka ya vifaa vya ufugaji wa nyuki hali ambayo huwalazimu kuagiza vifaa vya nyuki Tanzania Bara.

"Kuna tatizo la udanganyifu na uchakachuaji wa asali kwa baadhi ya wafanyabiashara wa asali ambapo hudanganya asali wanazouza kuwa ni asali ya Zanzibar wakati baadhi ya asali huwa si za Zanzibar," alisema.

Aliomba serikali kuwapatia elimu ya ufugaji wa nyuki ili kuendana na ufugaji wa kisasa na kuachana na ufugaji wa kizamani ambao una kazi kubwa lakini mavuno yake ni kidogo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA INAUZWA

PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL). KWA MAWASILIANO ZAIDI

**TUPIGIE:0677 111 333 AU 0758 112 332**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

## KUPOTEA KWA CHETI



**LIGHTNESS WISDOM MAMUYA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0255-0552** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **ST.CHRISTINA GIRL'S** mwaka **2014,** yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa ARU/ARU/RB/602731/2021**

116432302

## KUPOTEA KWA CHETI



**JESCA AUGUSTINE MOSHIRU** anatangaza kupotelewa na result slip ya kidato cha nne yenye index namba **S.0234/0006** iliyotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **MCF KILIMANJARO ACADEMY** mwaka 2020,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa DAR/TAB/RB/421738/21**

116431702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA LUSHOTO**
**YAH:MAOMBI NA 09/2021**
**SWAHIBU SALIMU HOZA………MUOMBAJI**
**DHIDI**
**MARTINI SINGANO**
**RAMADHANI RAJABU**
**RAMLA RAJABU………..MJIBU MAOMBI**

**POPOTE MLIPO**

SWAHIBU SALIMU HOZA amefungua shauri la ardhi na 09/2021 mbele ya baraza la ardhi na nyumba ya Lushoto.shauri husika limepangwa kutajwa tarehe tarehe 4/09/2021 saa3:30 asubuhi.hivyo basi mnatakiwa kuleta utetezi wenu kesi vinapatikana vinapatikana masijala ya wazi ya baraza la ardhi na nyumba (W) lushoto.endapo hamtotekeleza haya,shauri hili litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa dhidi yenu

Ofisi ya baraza zipo wazi karibu na jengo la posta

AMRI hii imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa baraza hili

**Leo tarehe 26 mwezi 08 mwaka 2021**

116432402

## KUUZA DHAMANA

**KAPALAMA INTERNATIONAL LIMITED** Sadiki Jabez Muze/Wiffred Silas Maleko tutauza dhamana yake aina ya Benz Mercedes kwa idhini tuliyopewa na Dagaa Microfinance Limited .

**Simu:0714 300 700/0758 536 060**

116432202

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**FREDRICK ISMAIL NKIRWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye jina la **KING LION INVESTMENT CO.LTD** aina ya **KINGLION** yenye namba za usajili **T827BTD.Engine No. KL257FMIB6127547. Chassis No. LWPPCJ3AXB6127547,** Aina ya **KING LION** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/407750/2021.**

116432902

**SHERIA YA USAJILI WA ARDHI(SURA 334)**
**KUSAJILIWA KWA HATI YA KUMILIKIN ARDHI**
**CHINI YA KIFUNGU NA.72**
**NAMBA YA HATI.064003/167**
**KIWANJA NA.23,KITALU 'BB'**
**SHINYANGA TOWNSHIP.**

**HATI NA.064003/167**
MMILIKI ALIYESAJILIWA:DEUSDEDIT MISANO of P.O. BOX 349 SHINYANGA
MWOMBAJI: BARTAZAR LAZARO LUKUBENIJA of P.O. BOX 407 SHINYANGA
ARDHI: L.O NO.85282, KIWANJA NA 23,KITAKU'BB' SERVICES INDUSTRY, MAJENGO SHINYANGA TOWNSHIP

**ARE: META ZA MRABA 2674**

Maombi ya kusajili mabadiliko ya umiliki chini ya kifungu na 72 yamewasilishwa kwetu
Ofisi inausudia kusajili mabadiliko hayo ya umiliki iwapo hakutakua na pingamizi kwa muda wa miezi sita (6) tokea tarehe ya taarifa hii.

MSAJILI WA HATI MSAIDIZI,
MKOA WA SHINYANGA

116433002

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF HOME AFFAIRS**
**IMMIGRATION DIVISION**

## OMBI LA URAIA WA TANZANIA

Telegramu: IMMIGRATION REGIONAL,
Telephone : 027-2751557
027-2752284
TeleFax 027-275228
REF. IMM/MS/DN/16315/VOLI
MKUR UGENZI WA MAGAZETI, MOSHI

THE OFFICE OF THE
IMMIGRATION OFFICER ,
P.O.BOX 1049
MOSHI
KILIMANJARO
Date: 16/07/2021



**HII NI TAARIFA KUWA:**

**BIBI PATIENCE JAHENDA MUSINGA** –BOX 1226 MOSHI KILIMANJARO
Ambaye picha yake imeonyeshwa hapo juu,anaomba uraia kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi .Yeye ni raia wa KENYA na Nchi atokayo ni KENYA.
Kazi yake /Shughuli zake ni Mama wa Nyumbani,
Anuani ya biashara zake
Ameishi nchini tangu 2013, Pia amewahi kuishi Mikoa ya Kilimanjaro tu.

Mtu yeyeto mwenye sababu za kupinga mwombaji asipewe uraia, atume taarifa yake ya maandishi iliyosainiwa kwa:

**KAMISHNA MKUU WA UHAMIAJI,**
**S.L.P 512,**
**DAR ES SALAAM.**
**Kny: AFISA UHAMIAJI MKOA,**
**KILIMANJARO**

116433302

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA MOSHI.**
**WILAYA YA MOSHI**
**MAOMBI NA. 87/2021**
**DAUDI BASHE HASHAN (suing as legal administrator of estates of the late Asha Mohamed Laban)…………………………………MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**HUSSAIN KHALIF HUSSEIN……………………………WAJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**
**KWA: HUSSAIN KHALIF HUSSEIN**

Kwa kuwa mdai ameleta madai ya kesi na yameelezwa katika nakala ya madai ambayo inapatikana katika Baraza la Ardhi na Nyumba Moshi. Shauri limepangwa kutajwa tarehe 04/10/2021 saa mbili na nusu (2:30) asubuhi mbele ya Mheshimiwa Mwenyekiti J.SILIAS, hivyo unatakiwa kufika mahakamani wewe au wakili wako .
ANGALIA: Kama hutahudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu Mahakama itasikiliza shauri hili na kutoa uamuzi upande mmoja.
Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 24 mwezi wa 8 , 2021.

**Mh: JAMES SILLAS**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI-MOSHI**

116433602

**KABANGO GENERAL BUSINESS (T) LTD**

**TANGAZO LA MNDA WA HADHARA**

**SHAURI LA UTEKELEZAJI NAMBA 317/2021**
**M/S HERITAGE HEIGHTS T/A BELAVISTA APPARTMENTS………MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

1. **M/S ROYAL PEONY INTERNATIONAL (T) LTD**
2. **ISSACK SAMWELI MJEMA**
3. **PAULINA MARRY MAYER……………….WAJIBU MAOMBI**

KWA AMRI NA IDHINI TULIYOPEWA NA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA KINONDONI INAYOTUAMURU KUUZA GARI AINA YA TOYOTA IST T114DRA KWA NJIA YA MNADA WA HADHARA UTAKAO FANYIKA TAREHE 14/09/2021 SAA NNE KAMILI ASUBUHI.

**MNADA UTAFANYIKA UWANJA WA UBUNGO MAKUBULI SHULENI KARIBU NA SERIKALI YA MTAA WA MAKUBURI**

**MASHARTI YA MNADA**

MNUNUZI ATAKAYESHINDA KATIKA MNADA ATATAKIWA KULIPA 25% PAPO HAPO KWA BEI ITAKAYOFIKIWA NA 75% ZITALIPWA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14), MNUNUZI AKISHINDWA KULIPA KIASI KILICHOBAKI NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14) PESA ILIYOTOLEWA HAITARUDISHWA NA MNADA UTARUDIWA.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA 0788 026933 / 0735 024068**

116433702

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Afrika Kusini yabaini aina mpya ya virusi vya corona

**Johanesburg,** AFRIKA KUSINI

WATAFITI wanachunguza aina mpya ya virusi vya corona, aina ya C.1.2, ambavyo huzaana mara mbili zaidi, havijatajwa kuwa vyenye kutia wasiwasi.

Matukio ya virusi hivyo yamerekodiwa katika kila mkoa Afrika Kusini pamoja na mataifa saba ya Afrika, Bara Asia, Ulaya na maeneo ya bahari.

**Taifa hilo limesajili maambukizi 2,770,575 ya virusi vya corona ikiwamo vifo 81,830.**

Wanasayansi wanatathmini jinsi aina hiyo ya virusi inavyokabiliana na viini vinavyopigana na corona. Pia wanachunguza jinsi vinavyozaana na maambukizi yake.

Maria van Kerkhove, ofisa wa kiufundi anayeongoza uchunguzi huo kwa niaba ya Shirika la Afya Duniani (WHO), alisema kwamba virusi hivyo havionekani vikiongezeka.

Alisema kwamba aina hiyo ya virusi ndio inayoendelea kuwaathiri wengi na kwamba WHO itaufahamisha umma iwapo kutakuwa na mabadiliko yoyote.

Afrika Kusini, ni taifa ambalo limeathiriwa vibaya na aina zote mbili za maradhi ya corona ikiwamo yale ya virusi vya Delta na Beta, ambayo yanasambazwa kwa urahisi zaidi.

Taifa hilo limesajili maambukizi 2,770,575 ya virusi vya corona ikiwamo vifo 81,830. **BBC**




Wapiganaji wa Taliban wakiwa mbele ya lango la kuondokea abiria wanaowasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Hamid Karzai baada ya majeshi ya Marekani kuandoka Kabul, Afghanistan, jana. **PICHA: AP**

## Maofisa wa Nigeria waomba msaada, wapiganaji Boko

**Abuja,** NIGERIA

MAOFISA wa Kaskazini mwa Nigeria wameomba msaada Serikali Kuu baada ya miezi ya hivi karibuni watu wapatao 3,000 kujisalimisha wakiwamo wanamgambo wa Boko Haram. Jeshi la Nigeria limesema hiyo ni ishara kwamba limefanikiwa kuwazidi nguvu wanamgambo wa kundi hilo la kijihadi katika mgogoro unaoendelea kwa miaka 12.

Wanamgambo hao pamoja na familia zao walianza kujisalimisha kufuatia kuuawa kwa kiongozi wa kundi hilo Abubakar Shekau mnamo mwezi Mei wakati wa mapigano na wapiganaji wa Tawi la Magharibi mwa Afrika la Dola la Kiislam (ISWAP).

Gavana wa Jimbo la Borno Babagana Zulum amesema wengi waliojisalimisha ni wanawake, watoto na wakulima ambao walilazimishwa kufanya kazi katika eneo ambalo lilikuwa likidhibitiwa na Boko Haram. **DW**

## 29 wafariki wakielekea visiwa vya Canary

**Canaray,** HISPANIA

WAAFRIKA wapatao 29, ikiwa ni pamoja na watoto saba, wamefariki dunia wiki iliyopita wakijaribu kuelekea katika visiwa vya Hispania vya Canary katika boti ndogo ya kusafirisha watu kimagendo.

Kwa mujibu wa ushuhuda wa manusura, miili ya wale ambao walikufa wakati wa safari ilitupwa baharini na wasafiri wenzao, lilisema Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM). Siku ya Jumatatu, boti za uokozi za Hispania, zilifanikiwa kuwaokoa wahamiaji 27 na kuopoa miili ya watu wanne, baada ya boti waliokuwamo ndani yake kuonekana na wavuvi Kusini mwa El Hierro, moja wapo ya visiwa vya Canary.

Boti hiyo iliondoka Agosti 15 mwaka huu, kutoka Dakhla, mji wa bandari katika Jangwa la Sahara Magharibi. **DW**

# Marekani yaharibu vifaa vyake vya kijeshi ikiondoka Afghanistani

**Kabul,** AFGHANISTAN

JESHI la Marekani lilihakikisha linaharibu ndege zao na magari ya silaha, waliyoyaacha kwenye uwanja wa ndege mjini Kabul, kabla ya kuondoka usiku wa Jumatatu. Maofisa wameeleza.

Kamanda wa Majeshi ya Marekani, Jenerali Kenneth McKenzie, alisema vikosi viliharibu ndege zake 73 na magari 70 ya silaha na mengine ya kijeshi, ili Taliban wasiweze kuyatumia.

"Ndege hizo hazitaweza kuruka tena...hakuna mtu yeyote atakayeweza kuyaendesha," alisema.

Video iliyotumwa na mwandishi wa habari wa Los Angeles, ilionyesha Taliban wakiingia kwenye uwanja wa ndege eneo ambao ndege za Marekani zimeegeshwa wakionekana kukagua vifaa hivyo. Pia Marekani imeelemaza mfumo wa roketi wa teknolojia ya juu uliachwa uwanja wa ndege.

Mfumo wa C-RAM ulifanya kazi Jumatatu kudhibiti shambulio la roketi la wanamgambo wa IS lililolenga uwanja wa ndege.

Awali, wapiganaji wa Taliban katika kipindi cha majuma kadhaa yaliyopita wameonekana wakiwa na vifaa vya kijeshi vya Marekani na vyombo vya moto.

Vifaa hivyo vilikuwa vimegawiwa kwa Jeshi la Afghanistan, baada ya jeshi hilo kuweka silaha chini, vifaa hivyo viliingia mikononi mwa Taliban. Ofisa mmoja wa ngazi ya juu wa Taliban Jumatatu aliiambia VOA kwamba, ndege ya mwisho ya wanajeshi wa Marekani imeondoka baada ya kukaa Afghanistan kwa miongo miwili.

Tangazo hilo lilikuja wakati ikulu ya Marekani pamoja na Pentagon wakiahidi kuendelea kuokoa Wamarekani pamoja na watu wa Afghanistan, walio hatarini nchini humo, ikisemekana kuwa uokozi mkubwa zaidi uliowahi kufanywa katika historia ya Marekani.

Wakati huo huo, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, juzi lilisema kwamba linatumai kwamba Taliban watahakikisha usalama wa watu wanaotaka kuondoka nchini humo.

Kati ya wanachama 15 wa baraza hilo, Russia na China hawakushiriki kwenye rasimu ya azimio hilo lililoandikwa na Marekani, Uingereza na Ufaransa na kuungwa mkono na mataifa mengine wanachama.

Baraza hilo liliangazia taarifa ya Taliban ya Agosti 27, mwaka huu, kwamba hawatazuia watu wa Afganistan wanaotaka kuondoka nchini, iwe ni kwa barabara au ndege.

Operesheni hii kubwa, ilioanza Agosti 14, imewezesha kuondoa watu zaidi ya 123,000, kulingana na takwimu za hivi karibuni zilizotolewa na makao makuu ya jeshi la Marekani, Pentagon. **BBC/RFI**

MECHI KALI

HOME



PORTUGAL

1.18 | 6.61 | 16.02

IRELAND



AWAY

1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4 - WEKA PESA.
vodacom m-pesa airtel money tigo pesa EZYPESA
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
halopesa
SEND

2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 468



# HENDERSON LIVERPOOL WAJIFUNGA HADI 2025

**LIVERPOOL,** England

NAHODHA wa Liverpool, Jordan Henderson, amesaini mkataba mpya wa miaka minne utakaomfanya abakie hapo hadi mwaka 2025.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, amecheza jumla ya mechi 394 kwa Liverpool tangu alipojiunga nayo kutoka Sunderland mwaka 2011 na aliteuliwa kuwa nahodha wa Liverpool mwaka 2015.

Henderson, ambaye alishinda taji la Ligi Kuu England, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la Ligi akiwa na Liverpool, alibakiwa na miaka miwili kwenye mkataba wake na sasa atakaa hapo Anfield hadi mwaka 2025.

Kiungo huyo wa timu ya Taifa ya England, amekuwa mchezaji mwingine mkubwa kusaini mkataba mpya baada ya Virgil van Dijk, Alisson, Fabinho, Trent Alexander-Arnold na Andrew Robertson kipindi hiki cha majira ya joto. Henderson ameiambia tovuti ya klabu hiyo kuwa: "Kwa uhakika najisikia heshima kubwa na ufahari kuendelea na safari hapa, sehemu ambayo nilikuwapo muda mrefu.

"Ni jambo la kushangaza kuona kwamba nimeweza kuwa hapa na kupata mafanikio makubwa, nina imani safari yangu itakuwa bora zaidi."



# Mbappe, Madrid kusaini Januari

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe anapanga kusaini mkataba wa awali wa makubaliano na Real Madrid Januari baada ya Paris Saint-Germain kushindwa kujibu ofa ya pauni milioni 154.4 iliyotolewa na miamba hao wa Ligi Kuu Hispania, kwa mujibu wa Sky Sport.

Real ilitoa ofa ya pili ya pauni milioni 145.8 ambayo PSG hawakujibu hadi jana siku ya mwisho ya kufungwa kwa pazia la dirisha la usajili.

Hata hivyo, Madrid wana uhakika wa kumsajili mchezaji huyo kwa uhamisho huru msimu ujao ambao mkataba wake wa sasa utakuwa umemalizika.

Mshambuliaji huyo wa Ufaransa alithibitisha Jumatatu kwamba, hatasaini mkataba mpya na PSG na sasa ataweza kuondoka akiwa huru.

PSG wamekuwa wakijaribu kumshawishi Mbappe kusaini mkataba mpya, lakini nyota huyo mwenye umri wa miaka 22, ameonyesha wazi kwamba hataki kubaki hapo.

## HABARI MICHEZO

,576,020

# JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/09/21 | 17:00 | Exeter vs Forest Green | 2.95 | 3.24 | 2.31 |
| 02. 04/09/21 | 17:00 | Carlisle vs Salford City | 2.65 | 2.95 | 2.75 |
| 03. 04/09/21 | 17:00 | Oldham vs Barrow | 2.45 | 3.19 | 2.79 |
| 04. 04/09/21 | 17:00 | Stevenage vs Swindon Town | 2.54 | 2.94 | 2.89 |
| 05. 04/09/21 | 17:00 | Newport vs Leyton Orient | 2.56 | 2.95 | 2.85 |
| 06. 04/09/21 | 17:00 | Colchester vs Sutton United | 2.38 | 3.03 | 3.03 |
| 07. 04/09/21 | 17:00 | Southend vs Wrexham | 2.54 | 3.22 | 2.63 |
| 08. 05/09/21 | 01:30 | Remo PA vs Botafogo RJ | 2.89 | 3.09 | 2.35 |
| 09. 05/09/21 | 03:00 | Bahia BA vs Fortaleza CE | 2.57 | 3.15 | 2.57 |
| 10. 05/09/21 | 03:00 | Cuiaba MT vs Santos | 2.36 | 3.11 | 2.86 |
| 11. 05/09/21 | 05:00 | San Jose Earthquake vs Colorado Rapids | 2.49 | 3.46 | 2.70 |
| 12. 05/09/21 | 19:15 | Mirandes vs Las Palmas UD | 2.62 | 2.81 | 2.96 |
| 13. 05/09/21 | 19:30 | Patronato Parana vs Talleres | 2.80 | 2.94 | 2.51 |


# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 01 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2785 | Urawa Red Diamonds vs Kawasaki Frontale | 4.54 | 3.62 | 1.67 |
| 13:00 | 2888 | Nagoya Grampus vs Kashima Antlers | 2.76 | 2.91 | 2.57 |
| 13:00 | 3133 | Cerezo Osaka vs Gamba Osaka | 2.07 | 3.20 | 3.34 |
| 14:15 | 4691 | Senja FK vs Eidsvold Turn | 3.78 | 3.98 | 1.73 |
| 15:00 | 1077 | Bristol City U23 vs Hull City U23 | 1.86 | 3.29 | 3.96 |
| 15:00 | 5910 | Moss vs Brattvag | 2.90 | 3.68 | 2.09 |
| 16:00 | 1406 | Fram Larvik vs Levanger | 2.56 | 3.77 | 2.27 |
| 16:00 | 2494 | Nardo vs Oeygarden FK | 2.71 | 3.43 | 2.30 |
| 16:00 | 5521 | Central African Republic vs Cape Verde | 3.63 | 3.05 | 2.03 |
| 17:00 | 2664 | Arendal vs Sotra SK | 1.26 | 5.62 | 8.14 |
| 17:00 | 4855 | Kazakhstan vs Ukraine | 6.99 | 4.09 | 1.49 |
| 18:00 | 2991 | Prerov vs SK Lisen | 9.68 | 6.58 | 1.19 |
| 18:00 | 3566 | Blansko vs Zlin | 7.54 | 5.41 | 1.29 |
| 18:00 | 4379 | MFK Vitkovice vs Fotbal Trinec | 3.73 | 4.36 | 1.67 |
| 18:00 | 5091 | FK Olympie Brezova vs Hradec Kralove | 12.54 | 7.72 | 1.13 |
| 18:15 | 1898 | KFUM Roskilde vs AB Gladsaxe | 3.48 | 3.53 | 1.91 |
| 18:15 | 2863 | Taarnby FF vs Lyngby | 22.29 | 11.63 | 1.04 |
| 18:15 | 3276 | Bredballe IF vs Middelfart | 27.17 | 11.64 | 1.03 |
| 18:15 | 3688 | Hillerod vs Sonderjyske | 9.27 | 5.60 | 1.24 |
| 18:30 | 2372 | Pif Jalkapallo vs Grankulla Ifk | 1.77 | 4.06 | 3.53 |
| 18:30 | 2887 | HJS Akatemia vs Vjs | 1.37 | 5.23 | 5.81 |
| 18:30 | 4359 | Brabrand IF vs Vendsyssel FF | 6.19 | 4.54 | 1.40 |
| 18:30 | 4444 | VPS Vaasa vs TPS Turku | 3.20 | 3.34 | 2.07 |
| 18:30 | 4891 | MP Mikkeli vs PK-35 | 2.17 | 3.34 | 3.00 |
| 19:00 | 1523 | Skeid Fotball vs Flekkeroy | 1.30 | 5.22 | 7.34 |
| 19:00 | 2876 | Hodd vs Floro | 1.21 | 6.01 | 9.69 |
| 19:00 | 3326 | Egersund IK vs Vard Haugesund | 1.86 | 3.82 | 3.39 |
| 19:00 | 4169 | Guinea Bissau vs Guinea | 3.81 | 2.94 | 2.03 |
| 19:00 | 4861 | Finland vs Wales | 2.95 | 3.05 | 2.55 |
| 19:00 | 5075 | Senegal vs Togo | 1.23 | 5.65 | 9.74 |
| 19:00 | 5481 | FC Roskilde vs Odense | 9.66 | 6.38 | 1.20 |
| 20:00 | 2029 | Baerum vs Kvik Halden | 3.53 | 3.73 | 1.84 |
| 20:00 | 4965 | Alta IF vs Kongsvinger IL | 2.56 | 3.63 | 2.33 |
| 20:00 | 5903 | IFK Luleaa vs Piteaa IF | 2.22 | 3.63 | 2.71 |
| 21:45 | 1686 | Slovenia vs Slovakia | 2.30 | 3.10 | 3.30 |
| 21:45 | 1901 | Switzerland vs Greece | 1.63 | 3.75 | 5.59 |
| 21:45 | 2990 | Latvia vs Gibraltar | 1.27 | 5.21 | 12.03 |
| 21:45 | 3010 | Norway vs Netherlands | 4.41 | 3.71 | 1.77 |
| 21:45 | 3023 | Portugal vs Ireland | 1.18 | 6.40 | 17.99 |
| 21:45 | 3131 | Faroe Islands vs Israel | 7.41 | 4.31 | 1.44 |
| 21:45 | 3175 | France vs Bosnia and Herzegovina | 1.18 | 6.61 | 16.02 |
| 21:45 | 3219 | Denmark vs Scotland | 1.44 | 4.31 | 7.41 |
| 21:45 | 3633 | Luxembourg vs Azerbaijan | 2.19 | 3.10 | 3.55 |
| 21:45 | 3808 | Qatar vs Serbia | 3.36 | 3.31 | 2.17 |
| 21:45 | 4140 | Turkey vs Montenegro | 1.49 | 4.11 | 6.81 |
| 21:45 | 4535 | Russia vs Croatia | 2.75 | 3.20 | 2.60 |
| 21:45 | 5082 | Malta vs Cyprus | 4.60 | 3.25 | 1.87 |
| 21:45 | 5366 | Moldova vs Austria | 15.00 | 6.00 | 1.21 |
| 22:00 | 1603 | Mali vs Rwanda | 1.54 | 3.49 | 6.21 |
| 22:00 | 2292 | Libya vs Gabon | 2.55 | 2.80 | 2.89 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# MAN UNITED YAIPIKU CHELSEA KWA NIGUEZ

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United ilikuwa mbele ya Chelsea katika mbio za kupata saini ya mchezaji wa Athletico Madrid, 'Los Rojiblancos' ya Hispania, Saul Niguez, kwa mujibu wa ripoti nchini Hispania.

Saul mwenye umri wa miaka 26, amekuwa akiwaniwa na timu kadhaa za Ligi Kuu England ikiwamo Liverpool. Lakini gazeti la kila siku la Hispania, AS limedai dili la mkopo likiwa na chaguo la kumnunua mchezaji huyo kati ya pauni milioni 34 na 40 linaweza kufanyika hivi karibuni huku uwezekano mkubwa ukiwa kutua Old Trafford.

Inaaminika mwanasoka huyo wa kimataifa wa Hispania ambaye yuko Los Rojiblancos tangu mwaka 2008 ana nia ya kutafuta changamoto mpya licha ya kuwa kwenye kikosi cha kwanza cha kocha Diego Simeone.

Athletico wanasemakana wanatoa ofa kwa timu za Ligi Kuu Uingereza kumsajili Saul wakati timu hiyo ikiwa kwenye jitihada za kupunguza bili ya mshahara ya klabu kwa lengo la kukamilisha usajili wa Matheus Cunha kutoka Hertha Berlin.



# Everton kumuachia Kean kurudi Juve

**LONDON,** England

EVERTON wameanzisha mazungumzo na Juventus kuhusu uwezekano wa mshambuliaji matata raia wa Italia, Moise Kean kujiunga upya na kikosi hicho cha kocha Massimiliano Allegri.

Haijabainika iwapo mpango huo utakuwa ni kwa mkopo au mkataba wa kudumu. Kean mwenye umri wa miaka 21, angali na miaka mitatu katika mkataba wake wa miaka mitano na Everton na alisajiliwa kutoka Juventus mwaka 2019.

Nyota huyo amechezeshwa mara mbili na Everton msimu huu wa 2021-22 chini ya kocha Rafael Benitez japo alionyeshwa kadi nyekundu katika mechi ya Kombe la Ligi dhidi ya Huddersfield Town Agosti 24, 2021.

Baada ya kuifungia Everton mabao mawili pekee katika mechi 33 za msimu wa kwanza, Kean alitolewa Paris Saint-Germain (PSG) ya Ufaransa kwa mkopo. Akiwa huko, alipachika wavuni mabao 16 kutokana na mechi 36 alizocheza.

Juventus kwa sasa hawana mshambuliaji tegemeo tangu Cristiano Ronaldo aagane nao na kurejea upya kambini mwa Manchester United ya Ligi Kuu England (EPL).

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI ULAYA




# RONALDO KUZOA MABILIONI MIAKA MIWILI MAN UNITED

Nyota huyo aliyefunga mabao 118 katika mechi 292 alizoichezea klabu hiyo, tayari amesaini...

**MANCHESTER,** England

CRISTIANO Ronaldo amesaini rasmi na Manchester United mkataba wa miaka miwili huku kukiwa na kipengele cha kuongeza mwaka mmoja.

United ilitangaza kufikia makubaliano na Juventus kwa ajili ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36, Ijumaa na kumfanya nyota huyo wa kimataifa wa Ureno kurudi tena Old Trafford.

**Miamba hao wa Ligi Kuu England watamlipa Ronaldo kiasi cha pauni milioni 12.9 pamoja na nyongeza ya bonasi pauni milioni 6.9, ambaye alikamilisha vipimo vya afya jijini Lisbon nchini Ureno wikendi.**

Ronaldo alifunga mabao 118 katika mechi 292 alizoichezea United kati ya mwaka 2003 na 2009, akishinda mataji matatu ya Ligi Kuu England, Kombe moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya, FA na mataji mawili ya ligi.

Ronaldo sasa kinachosubiriwa ni utambulisho wake pekee. United walieleza kuwa wamefikia makubaliano mazuri na Juventus ambapo alikuwa anacheza mshambuliaji huyo mwenye miaka 36 kwa ajili ya kuipata saini yake.

Nyota huyo anakwenda kurejea kwenye Ligi Kuu England anatajwa kuwekewa mkwanja mrefu na atakuwa anapokea pia mshahara mnono kwa wiki jambo ambalo lilimfanya akubali kurejea hapo.

## ZISIKUPITE

### MADRID YAJITOA KWA MBAPPE

REAL Madrid imejiondoa katika mazungumzo ya kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa Kylian Mbappe, 22, kutoka Paris St-Germain kwa sababu klabu hizo zimeshindwa kukubaliana. ***(RMC Sport)***

### CAMAVINGA RASMI MADRID

REAL Madrid imeipiku PSG katika mbio za kumsajili kiungo wa Ufaransa, Eduardo Camavinga, 18, kutoka Rennes. ***(Canal+ via Get French Football News)***

### MAN CITY HAISAJILI

KLABU ya Manchester City haitaruhusu mchezaji yeyote zaidi ama kuingia au kuondoka kabla ya dirisha la uhamisho kufungwa baada ya kumpa mkapata mpya Ederson, 28. ***(Times)***

### BELLERIN KUSAJILIWA BARCA

BARCELONA watajaribu kumsajili beki wa kulia wa Arsenal na Hispania, Hector Bellerin mwenye umri wa miaka 26, ikiwa mlinzi wa Brazil, Emerson Royal, 22, ataondoka Nou Camp na kujiunga na Tottenham. ***(Mundo Deportivo)***

### TAGLIAFICO KUTUA WEST HAM

KLABU ya West Ham imefikia makubaliano ya mdomo na Ajax kumsaini beki wao wa kushoto, Nicolas Tagliafico, 28. (Telegraaf)

### MAN UNITED NA KOUNDE

MLINZI wa Sevilla, Mfaransa Jules Kounde, 22, ameibuka kuwa mchezaji wa juu anayelengwa zaidi na Manchester United. ***(Mail)***

### CHELSEA NAO WAJITOSA

CHELSEA wamemwambia wakala wa beki wa kati wa Sevilla na Ufaransa, Jules Kounde, 22, watafanya jaribio la mwisho kumsajili mchezaji huyo. ***(ABC Sevilla, via Sport Witness)***

### TRAORE AITAKA TOTTENHAM

MSHAMBULIAJI wa Wolves, Adama Traore, 25, amemwajiri wakala Jorge Mendes kumsaidia kupata uhamisho wa kwenda Tottenham Hotspurs. ***(Footballer Insider)***

### LEICESTER WAMTAKA ODOI

KLABU ya Leicester City imeonyesha nia kwa winga wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi, 20, ambaye amehusishwa na Borussia Dortmund. ***(football.london)***

### NIGUEZ KWA MKOPO CHELSEA

CHELSEA wanataka kumchukua kiungo wa Atletico Madrid raia wa Hispania, Saul Niguez, 26, kwa mkopo. ***(Goal)***

### ROBERTS ATAKIWA BURNLEY

KLABU ya Burnley ipo kwenye mazungumzo ya kumleta mlinzi wa Swansea City na Wales Connor Roberts, 25, pale Turf Moor. ***(WalesOnline)***

## HABARI MICHEZO

# MAGORI: HUYU BEKI MKONGO WA SIMBA ATAIMBWA SANA

**Na Adam Fungamwango**

MJUMBE wa Kamati ya Usajili ya Simba na mshauri wa Mwenyekiti wa Bodi ya Klabu hiyo, Crescentius Magori, ameusifia usajili wa klabu hiyo kwa kusema umelenga wachezaji watakaoitoa klabu hiyo kutoka hapo ilipo na kuipandisha juu kwenye medani ya soka Afrika, huku akitaja usajili wa beki Henock Inonga Baka 'Varane', kutoka Motema Pembe ya Jamhuri ya Kidemkorasi ya Congo kuwa ndiyo usajili bora zaidi msimu huu nchini Tanzania.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Magori ambaye aliwahi kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, alisema beki huyo ni mmoja kati ya mabeki bora kabisa barani Afrika, anayeichezea timu ya Taifa ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na amecheza mechi nyingi za kimataifa, hivyo anaamini ipo siku wanachama na mashabiki wa Simba wataimba jina lake.

"Huyu beki ana kila kitu kinachohitajika kwa beki mzuri. Ana 'kontroo', ana uwezo wa kupiga chenga na kupunguza hata wachezaji wawili. Anaweza kucheza beki wa kati na kiungo mkabaji, ana uwezo wa kupiga miguu yote miwili. Ni mpambanaji na ana uwezo wa kuzuia chini pamoja na mipira ya juu.

**"Kusema kweli ni kwa sababu Watanzania hawajamuona, lakini akianza kucheza Ligi Kuu ya hapa, kuna siku mashabiki na wapenzi wa Simba wataimba jina lake," alisema Magori.**


Kuhusu usajili wa wachezaji wengine, Magori alisema kuwa ilichofanya klabu ya Simba ni kusajili wachezaji ambao wataitoa kwenye hatua ya robo fainali ambayo imekuwa ikiishia miaka ya karibu na kuelekea hatua ya nusu fainali na kuendelea.

"Kuna Pape Ousmane Sakho huyo, Kuna Duncan Nyoni, kuna Peter Banda, kuna mtu mmoja mrefu pale katikati kama 'antena', anaitwa Sadio Kanoute, yaani hiyo siku ya Simba Day watu watafaidi soka na siyo tamasha," alisema Magori.

Simba inajiandaa na Simba Day ambayo huifanya kila mwaka kabla ya kuanza kwa msimu mpya wa Ligi Kuu na michuano mingine.

Magori aligusia kuwa timu itakayocheza na Simba ni ile ambayo ipo kwenye zile timu 10 bora ambazo hazitacheza mechi za awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

## NAKUKUBALI FUNDI...



Msemaji wa Klabu ya Yanga, Haji Manara, akimfunga kamba za viatu, kiungo wa timu hiyo, Feisal Salum 'Fei Toto', kuonyesha anaukubali uwezo wake, wakati wa Kilele cha Siku ya Mwananchi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Waziri Junior ajifunga Dodoma Jiji*

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Dodoma Jiji FC, umemalizana na aliyekuwa mshambuliaji wa Yanga, Waziri Junior, baada ya kusaini mkataba wa kuitumikia timu hiyo kwa msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara, utakaoanza Septemba 29, mwaka huu.

Waziri amemwaga wino Dodoma Jiji FC, baada ya kuvunja mkataba wake na Yanga kutokana na kukosa nafasi ya kucheza ndani ya kikosi cha timu hiyo aliyotumikia kwa msimu mmoja akitokea Mbao FC.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Dodoma Jiji FC, Fortunatus John, alisema usajili wa nyota huyo ni miongoni mwa mapendekezo ya benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Mkuu, Mbwana Makata.

Alisema Waziri atakuwa miongoni mwa wachezaji wapya ndani ya timu hiyo na kwenda kuimarisha kikosi cha chao ambacho tayari kimeingia kambini kujiandaa na maandalizi ya msimu mpya wa ligi hiyo.

"Timu iko Morogoro ikifanya mazoezi yake katika Uwanja wa Chuo cha Ualimu mkoani humo, itakaa siku 14 na kuhusu mechi za kirafiki bado hatujapata taarifa yoyote kwa sababu kocha alihitaji kupata sehemu ya utulivu kwa ajili ya maandalizi ya kikosi chake," alisema Fortunatus.

Alisema kwa sasa wanasubiri program za benchi hilo la ufundi kuhusu mechi za kirafiki, na kwamba moja ya mikakati waliyompa kocha huyo ni kuhakikisha timu hiyo inamaliza katika nafasi nne za juu kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Tunatambua msimu huu utakuwa wa ushindani mkubwa, tumejipanga vizuri na tayari tumeshamweleza Kocha Makata mipango yetu na tunahitaji msimu huu kumaliza katika nafasi za juu," alisema katibu huyo.

## TFF yafunga dirisha la usajili Ligi Tanzania

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limefunga rasmi dirisha la usajili kwa timu za Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara na Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara.

Ofisa Habari wa TFF, Cliford Ndimbo amesema dirisha hilo limefungwa Agosti 31, na hakutokuwa na nyongeza kama ilivyokuwa misimu miwili au mitatu iliyopita.

"Tuna misimu miwili au mitatu sasa, dirisha likishafungwa halifunguliwi, klabu zilitakiwa kukamilisha usajili kwa wakati, hadi linaelekea kukamilika, klabu zote za Ligi Kuu zilikuwa zimekamilisha kufanya usajili, ila klabu mbili za Ligi Daraja la Kwanza pamoja na mbili za Ligi ya Wanawake ndiyo zilikuwa bado, lakini naamini hadi muda ule ambao linafungwa watakuwa wameshakamilisha. Ni kweli kulikuwa na changamoto, lakini klabu zilitoa taarifa na kupata msaada kutoka TFF," alisema Ndimbo.

Kwa upande wa Kagera Sugar dakika za mwisho, ilikamilisha usajili wa kipa raia wa Burkina Faso, Nurdin Balora, ambaye msimu uliopita alikuwa akiidakika Namungo FC, pamoja na Bolton Omwenga kutoka Nairobi City Stars ya Kenya.

## BMT yatoa neno kwa wagombea CHANETA

**Na Saada Akida**

BARAZA la Michezo la Taifa (BMT), limewataka wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi wa Chama cha Netiboli nchini (CHANETA), kuzingatia vigezo vilivyowekwa, lengo likiwa ni kuwezesha kupatikana viongozi sahihi.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Ofisa Uhusiano wa BMT, Najaha Bakari, alisema sifa zinazozingatiwa kwa wagombea ni pamoja na uraia wa mgombea kuwa Mtanzania na awe na ufahamu mzuri wa mchezo huo.

Aidha, ametoa wito kwa wagombea wanaowania nafasi ya mwenyekiti, katibu, mweka hazina pamoja na wajumbe sita (6) wa kuchaguliwa, kuwa ni mwenye elimu ya kidato cha nne ama zaidi huku kwa nafasi za wajumbe wagombea wajue kusoma na kuandika.

Fomu za uchaguzi zilianza kutolewa tangu Agosti 23 huku mchakato huo ukitarajiwa kukoma Oktoka 12 na kisha uchaguzi kufanyika Oktoba 15, mwaka huu jijini Dodoma.

Michezo
Jumatano Septemba 1, 2021
Nipashe



Ronaldo kuzoa mabilioni Man Utd UKURASA 22

# SIMBA DAY NI AL AHLY, MAMELODI KWA MKAPA

## ●●● Rais CAF naye kualikwa huku uongozi ukiahidi soka la...

**Na Saada Akida**

BAADA ya juzi Klabu ya Simba kueleza kwamba shughuli zote za matamasha ambazo zimeshuhudiwa nchini ni kama 'kitchen party', na kwamba harusi kamili ni Septemba 19, mwaka huu, ni wazi miamba hiyo ya soka nchini haitanii kwani ipo tayari Simba Day kuwashusha mabingwa wa Afrika kucheza mechi ya kirafiki Uwanja wa Benjamin Mkapa, imeelezwa.

**Kaimu Ofisa Habari wa Simba, Ezekiel Kamwaga, alisema Septemba 19, watafanya tamasha la wakubwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, baada ya watoto kutangulia na kumaliza shughuli yao.**

“Wanachama na mashabiki wa Simba sasa wakae mkao wa kula, ngoma za watoto zimeisha, yaliyofanyika juzi yalikuwa ni kama 'kitchen party' tu, harusi yenyewe itakuwa Septemba 19, ndiyo sasa itakuwa shughuli ya wakubwa,” alisema Kamwaga.

Lakini kwa mujibu wa Mjumbe ya Kamati ya Usajili na Mshauri wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba Mohamed Dewji, Crescentius Magori, alisema Simba Day wanaleta timu kubwa ambayo iko katika nafasi 10 za juu katika ukanda huu wa Afrika.

Alisema siku hiyo itakuwa ni ya kuvutia zaidi kuwahi kutokea nchini na kuwataka mashabiki wajitokeze kwa wingi uwanjani kwa sababu wanaleta timu kubwa ambayo watakipa mazoezi kikosi cha Simba kujiandaa na mechi zilizopo mbele yao.

“Baada ya mapumziko mafupi timu inaendelea na kambi nje ya jiji huku ikicheza mechi mbili za kirafiki na itarejea kwa ajili ya kucheza mechi ya tano ya kimataifa ya kirafiki dhidi ya timu kubwa hapa Afrika.

“Sisi tumejipanga na Siku ya Simba [Simba Day] itakuwa ya kipekee itakayotoa burudani pamoja na kutoa maandalizi mazuri kwa timu. Sisi Simba ni timu ya mpira na si kwa ajili ya matamasha,” alisema Magori

Hata hivyo, wakati viongozi wa Simba wakifanya siri kubwa kuhusu timu itakayokuja kucheza mechi ya kirafiki siku hiyo, mjumbe mmoja wa Kamati ya Utendaji ndani ya klabu hiyo, aliliambia gazeti hili kuwa, wamepanga kuwaleta mabingwa wa Afrika, Al Ahly ya Misri ama mabingwa wa zamani wa michuano hiyo, Mamelodi Sundowns FC ya Afrika Kusini.

“Tayari tupo katika mazungumzo na timu hizo, mojawapo itakuja kucheza mechi ya kirafiki Simba Day, lakini ikiwezekana Patrice Motsepe [Rais wa Shirikisho la Soka Afrika-CAF) kuwa mgeni rasmi wa tamasha hilo kubwa ambalo litakuwa la aina ya kipekee,” alisema mjumbe huyo.

Hii haitokuwa mara ya kwanza kwa shughuli za michezo ya Simba kuwaalika viongozi wakubwa kisoka Afrika, kwani mwaka juzi katika mchezo wao wa Ligi Kuu dhidi ya Yanga ilipata ugeni mkubwa baada ya kuhudhuriwa na Rais wa CAF aliyepita, Ahmad Ahmad

Simba iliweka kambi ya wiki tatu katika Jiji la Rabat, nchini Moroco kwa ajili ya kujiwinda na msimu mpya wa michuano ya kimataifa na Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajiwa kuanza kutimua vumbi Septemba 29, mwaka huu.

Hata hivyo, timu hiyo itakuwa na kibarua pevu dhidi ya Yanga kwenye mechi ya Ngao ya Jamii Septemba 25, mwaka huu ambayo itakuwa rasmi kwa ajili ya kufungua pazia la Ligi Kuu msimu huu wa 2021/22.




Beki kisiki wa Simba, Henock Inonga Baka 'Varane'.
**HABARI UK. 23**

## Senzo sasa apewa ubosi rasmi Yanga

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Yanga umemtangaza rasmi Senzo Mbatha Mazingisa, kuwa Kaimu Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, ikiwa ni hatua ya utekelezaji wa maadhimio ya mabadiliko ndani ya klabu hiyo akichukuwa nafasi ya Haji Mfikirwa.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema Senzo ameongezewa cheo na kuchukuwa nafasi hiyo ya Mfikirwa ambaye naye amerudia katika nafasi yake ya fedha na utawala.

Alisema malengo makubwa ya mabadiliko hayo ni kutekeleza maadhimio ya mkutano mkuu katika kuhakikisha wanaingia katika mabadiliko na klabu kuendeshwa kisasa.

“Sasa tunatekeleza yale maadhimio ya mkutano mkuu, katika mabadiliko hayo ya kuifanya klabu ya Yanga kuwa bora Afrika, Senzo atakuwa Mtendaji Mkuu na kutekeleza yale yote ya ndani ya klabu,” alisema Mwakalebela.

Alisema kuhusu kikosi cha timu hiyo kinaendelea vizuri na wanaendelea na mazoezi mara mbili kwa siku, asubuhi na jioni ikiwa ni maandalizi ya mchezo wao wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Rivers United ya Nigeria.

Mwakalebela alisema wako katika mpango wa kupata timu kutoka nje ya Tanzania ambazo watacheza mechi ya kirafiki kabla ya Septemba 12, mwaka huu kuikaribisha na Rivers United.

“Tayari tumeshaanza maombi ya timu ili kupata mechi za kirafiki, mbali na ile tuliyocheza katika Siku ya Wananchi, kujipima kuelekea mchezo wetu wa kimataifa,” alisema Mwakalebela.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042